zaidi ya hao.I hope next year ['the year which  
comes'] more will fly than that.Sangai

~gumu

hard, difficult

gharama (N)

expense, outlay

Kumbuka ni vigumu sana kupata pesa  
za kulipa gharama.Remember it is very hard to get the  
money to pay the expenses.

NotesA. Relative counterparts of the a-tense.

mwaka ujao	the year which comes
miezi ijayo	months which come
mtu aliye na njaa	a person who is hungry

These relative forms (cf. Unit 68) are all formed with subject prefix, plus stem (-ja or -li), plus relative affix. The first two examples illustrate relative counterparts of the a-tense.

2.

## A. Multiples of ten.

10	Wanafunzi kumi walikwenda Ulaya mwaka jana.	Ten students went to Europe last year.					
20	Wanafunzi ishirini walikwenda Ulaya mwaka jana.	Twenty students went to Europe last year.					
30	40	50	60	70	80	90	100

## B.

12	Mwalimu mkuu wa shule amenunua vikombe kumi na viwili.	The head teacher has bought twelve cups.					
22	Mwalimu mkuu wa shule amenunua vikombe ishirini na viwili.	The head teacher has bought twenty-two cups.					
32	42	52	62	72	82	92	102

C. Relative counterpart of the a-tense.

mwaka	Ninataka kusoma vitabu vingi mwaka ujao.	I want to read many books next year.
miaka	Ninataka kusoma vitabu vingi miaka ijayo.	I want to read many books in the years to come.
mwezi	Ninataka kusoma vitabu vingi mwezi ujao.	I want to read many books next month.

miezi	Ninataka kusoma vitabu vingi miezi ijayo.	I want to read many books in the months to come.
siku	Ninataka kusoma vitabu vingi siku zijazo.	I want to read many books in the days to come.

## D.

15	Kila mwanafunzi atapata zaidi ya vitabu kumi na vitano.	Every student will get more than fifteen books.				
25	Kila mwanafunzi atapata zaidi ya vitabu ishirini na vitano.	Every student will get more than twenty-five books.				
35	45	55	65	75	85	95
105	Kila mwanafunzi atapata zaidi ya vitabu mia (moja) na vitano.	Every student will get more than a hundred and five books.				
125	Kila mwanafunzi atapata zaidi ya vitabu mia (moja) na ishirini na vitano.	Every student will get more than a hundred and twenty-five books.				

## 3.

## A. Concord, including the last word in a numeral phrase.

chupa	Leo tumeuza chupa ishirini na tano za soda. Jana tuliuzza zaidi (ya hizo).	Today we have sold twenty-five bottles of soda. Yesterday we sold more than that.
taa	Leo tumeuza taa ishirini na tano. Jana tuliuzza zaidi (ya hizo).	Today we have sold twenty-five lamps. Yesterday we sold more than that.
mayai	Leo tumeuza mayai ishirini na matano. Jana tuliuzza zaidi (ya hayo).	Today we have sold twenty-five eggs. Yesterday we sold more than that.
mananasi	Leo tumeuza mananasi ishirini na matano. Jana tuliuzza zaidi (ya hayo).	Today we have sold twenty-five pine- apples. Yesterday we sold more than that.



mikate	Leo tumeuza mikate ishirini na mitano. Jana tuliuzza zaidi (ya hiyo).	Today we have sold twenty-five loaves of bread. Yesterday we sold more than that.
visu	Leo tumeuza visu ishirini na vitano. Jana tuliuzza zaidi (ya hivyo).	Today we have sold twenty-five knives. Yesterday we sold more than that.
vitabu	Leo tumeuza vitabu ishirini na vitano. Jana tuliuzza zaidi (ya hivyo).	Today we have sold twenty-five books. Yesterday we sold more than that.

B. Li-tense: affirmative vs. negative.

kuingia	Hasani aliingia nyumbani. Daudi hakuingia.	Hasani entered the house. Daudi didn't enter.
kukata	Hasani alikata tamaa. tamaa Daudi hakukata tamaa.	Hasani despaired. Daudi didn't despair.
kuañkia	Hasani alituankia. Daudi hakutuankia.	Hasani welcomed us. Daudi didn't welcome us.
kuendelea	Hasani aliendelea na masomo. na Daudi hakuendelea. masomo	Hasani continued with school. Daudi didn't continue.
kuhamishwa	Hasani alihamishwa na serikali. Daudi hakuhamishwa.	Hasani was moved by the government. Daudi wasn't moved.

Unit 70

1. Basic Dialogue. A day off.

Sangai

furaha (N)

rejoicing

Leo ni Jumamosi, siku ya furaha!

Today is Saturday, a day of rejoicing.

Abasi

mipango (MI)

plan, manner, method

Tena! Una mipango yo yote?

Right! Do you have any plans?

Sangai

sinema (N) (or: senema (N))

cinema

Twende sinema leo jioni.

Let's go to the movies this evening.

Abasi

ngoma (N)

drum

Haya. Halafu tutakwenda ngomani.

O.K., and then we'll go to watch the dances.

Sangai

Ndiyo, mimi napenda ngoma sana.

Yes, I like the dances very much.

Abasi

-cheza

to play

dansi (N)

dance

Mimi pia, ijapokuwa siwezi kucheza vizuri.

Me too, even though I can't dance well.

2.

## A. Days of the week.

Sat. Tutajaribu kukutembelea We'll try to visit you next  
Jumamosi ijayo. Saturday.

Sun. Tutajaribu kukutembelea We'll try to visit you next  
Jumapili ijayo. Sunday.

Monday-Jumatatu Tuesday-Jumañine Wednesday-Jumatano

Thursday-Alhamisi Friday-Ijumaa

## B.

Fri. Hamisi amekuwa (po) hapa Hamisi has been here since Friday.  
tangu Ijumaa.

Sat. Hamisi amekuwa (po) hapa Hamisi has been here since  
tangu Jumamosi. Saturday.

Sunday Monday Tuesday Wednesday Thursday

3.

A. Ta-tense: affirmative vs. negative, with person change.

Utakwenda sinema Jumamosi Are you going to the cinema next  
ijayo? Saturday?

Hapana, sitakwenda. No. I won't go.

Utaangusha sahani zote! You will drop all the plates.

Hapana, sitaziangusha. No. I won't drop them.

Utamwaga mafuta! You will spill the oil.

Hapana, sitayamwaga. No. I won't spill it.

Mafuta yatamwagika! The oil will be spilled.

Hapana, hayatamwagika. No. It won't be spilled.

Utaharibu kalamu yangu! You will spoil my pen.

Hapana, sitaiharibu. No. I won't spoil it.

Kalamu itaharibika!

The pen will be spoiled.

Hapana, haitaharibika.

No. It won't be spoiled.

4. A is a student in night school. B is thinking about attending, and asks A about it.

C is the father of three children who are of school age. D has five. They discuss the problems involved in the elementary education of their children.

## Reading Selection II

Vyakula vya Afrika ya Mashariki

Katika Afrika ya Mashariki vyakula vitatu hutumiwa sana zaidi ya vingine na wenyeji. Upande wa Uganda, 'matoke' ndicho chakula kikuu. Ndizi huchemshwa halafu huondwa kwa mwiko mpaka ziwe kama viazi vilivyopondwa.

Ugali, ni unga wa mahindi au wa mtama unaochanganywa na maji yanayochemka. Huu hufanana na uji lakini ugali ni mkavu zaidi kuliko uji. Unga hupatikana kutoka katika mahindi yaliyosagwa. Ili chakula chenyewe kiwe kitamu, ugali huliwa na kitoweo cha nyama au mboga na mchuzi. Wajaluo ndio walioanza kupika ugali.

Kama vile wenyeji wa bara wanavyosifu ugali, vivyo ndivyo watu wa pwani wanavyosifu wali. Waarabu wanajulikana sana kwa kula wali. Mchele ukiwa na maganda huitwa mpunga, na bila maganda kabla haujapikwa, mchele, lakini ukisha kuwa tayari kwa kula ni wali.

mwenyeji (WA)	the regular possessor; inhabitant	-changanya	to mix
		-fanana	to resemble one another
matoke (pl. MA)	name of a type of food	~kavu	dry
ndicho	that is it, (sg. VI class)	-saga	to pulverize
-chemsha	to cause to boil	ili	in order that
-ponda	to crush by pounding	~tamu	sweet, pleasant delicious
mwiko (MI)	a large wooden spoon	kitoweo (VI)	a relish
ugali (U)	stiff porridge	mchuzi (MI)	gravy, soup, sauce
unga (U)	flour, meal	ndio	it is they, (plu. WA class)
mtama (MI)	millet	-pika	to cook

bara (N)	the hinterland	wali (U)	cooked rice
-sifu	to praise	maganda (MA)	husks
-julikana	to be known	kabla (N)	before

Questions and Answers over Reading Selection

Questions

1. Vyakula vingapi hutumiwa sana katika Afrika ya Mashariki?
2. Vyakula hivyo ni vipi?
3. Nani wanaotumia vyakula hivi zaidi?
4. Matoke hupatikana wapi?
5. Utatumia nini kuponda ndizi?
6. Ni unga gani unaotumiwa kwa kupika ugali?
7. Unga na maji yanayochemka hufanywaje?
8. Ugali hufanana na uji?
9. Unga hupatikana kutoka wapi?

Sample Answers

- Vyakula vitatu.
- Vyakula hivyo ni matoke, ugali na wali.
- Wenyeji hutumia vyakula hivi zaidi.
- Matoke hupatikana katika nchi ya Uganda.
- Nitatumia mwiko.
- Unga wa mahindi, au wa mtama.
- Unga na maji yanayochemka huchanganywa.
- Ndiyo, lakini ugali ni mkavu zaidi kuliko uji.
- Unga hupatikana kutoka katika mahindi.

10. Namna gani? Mahindi husagwa.
11. Ugali ni chakula kitamu? Ndiyo, ugali ni chakula kitamu.
12. Ugali huchanganywa na nini? Ugali huchanganywa na kitoweo na  
mchuzi.
13. Wenyeji wa pwani wanasifu nini? Wanasifu wali.
14. Ni watu gani wanaojulikana sana waarabu.  
kwa kula wali?
15. Mchele ukiwa shambani huitwaje? Mchele ukiwa shambani huitwa mpunga.
16. Wali ni mchele wa namna gani? Wali ni mchele uliopikwa.

Unit 71

1. Basic Dialogue. Let's visit the farm.

Mirambo

shamba (MA)

farm

Tafadhali twende tukatembee

Please let's go take a walk around

shambani.

the farm.

Hasani

baada (N)

after

Ndiyo. Tutakwenda baada ya saa moja

Fine. We'll go in about an hour.

hivi.

-----

Hasani

-pita

to pass

Saa moja imepita. U tayari? (or:

An hour has passed. Are you ready?

Uko tayari?)

Mirambo

Ndiyo, ni tayari. (or: niko tayari.)

Yes, I'm ready.

Twende basi.

Well, let's go.

Hasani

-tangulia

to lead

njia (N)

path

-fuata

to follow

Tangulia. Nitakufuata. Unaijua

[You] lead [the way]. I'll follow

njia kuliko mimi.

you. You know the way better than

I do.



Mirambo

Haya, twende basi.

O.K., let's go then.

NotesA. Further example of the meaning of -ka-.

Tutembee shambani.

Let's take a walk on the farm

[beginning right where we are now].

Tukatembee shambani.

Let's [go] take a walk on the farm

[beginning from some point away from here].

The above examples provide another instance of the meaning of the prefix -ka-.

B. hivi 'about'

baada ya saa moja

after an hour

baada ya saa moja hivi

after about an hour

The word hivi, which in its shape is identical with the proximal demonstrative of the plural of the VI class, is in this sentence a modifier of saa moja, with the translation 'about'.

2.

## A. 'last' with days of the week.

Sun. Ulikuwa wapi Jumapili  
iliyopita?

Where were you last Sunday?

Mon. Ulikuwa wapi Jumatatu  
iliyopita?

Where were you last Monday?

Tuesday      Wednesday      Thursday      Friday      Saturday

B. Verb phrase with -wa; 'last year?'

wewe Ulikuwa ukifanya kazi gani  
mwaka uliopita?

What type of work were you doing last  
year?

ninyi	Mlikuwa mkifanya kazi gani mwaka uliopita?	What type of work were you (pl.) doing last year?
Bw. Sangai	Bw. Sangai alikuwa akifanya kazi gani mwaka uliopita?	What type of work was Mr. Sangai doing last year?
wanafunzi hawa	Wanafunzi hawa walikuwa wakifanya kazi gani mwaka uliopita?	What type of work were these students doing last year?

C. njia ya plus infinitive.

soko	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda sokoni.	Please, show me the way (to go) to the market.
hospitali	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda hospitalini.	Please, show me the way to the hospital.
boma	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda bomani.	Please, show me the way to the administrative office.
kanisa	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda kanisani.	Please, show me the way to the church.
hoteli	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda hotelini.	Please, show me the way to the hotel.
nyumba	Tafadhali, nionyeshe njia ya kwenda nyumbani.	Please, show me the way to the house.

3.

A. Infinitive vs. past negative.

kuja	Juma na Hasani waliahidi kuja mwezi uliopita, lakini hawakuja.	Juma and Hasani promised to come last month, but they didn't.
kwenda	Juma na Hasani waliahidi kwenda masomo ya jioni mwezi uliopita, lakini hawakwenda.	Juma and Hasani promised to go to the evening classes last month, but they didn't.

kuletea	Juma na Hasani waliahidi kuniletea barua mwezi uliofita, lakini hawakuniletea.	Juma and Hasani promised to send me a letter last month, but they didn't.
kusalimia	Juma na Hasani waliahidi kunisalimia mwalimu wao mwezi uliofita, lakini hawakunisalimia.	Juma and Hasani promised to convey my best regards to their teacher last month, but they didn't.

B. Simple vs. applied stem; 'every' vs. 'last' Saturday.

Sat.	Naandika barua kwa wazazi wangu kila Jumamosi. Niliwaandikia barua Jumamosi iliyopita.	I write to my parents every Saturday. I wrote them last Saturday.
Mon.	Naandika barua kwa wazazi wangu kila Jumatatu. Niliwaandikia barua Jumatatu iliyopita.	I write to my parents every Monday. I wrote them last Monday.

Wednesday      Thursday      Friday

Unit 72

1. Basic Dialogue. The farm needs rain and fertilizer.

Mirambo

-nyesha to rain

mavuno (MA) harvest

Mvua ikinyesha nitapata mavuno If it rains, I'll get a large harvest.  
mengi.

Hasani

Umepanda mimea gani shambani mwako? What kind of plants have you planted  
on your farm?

Mirambo

Viazi ulaya. Irish potatoes. ('European potatoes')

ningalikuwa if I were

mbolea (N) fertilizer

Kama ningalikuwa na mbolea If I had had fertilizer, I would have  
ningalipanda vitunguu. planted onions.

Hasani

-agiza to order

Unaweza kuiagiza kutoka Idara ya You can order it from the Department  
Ukulima. of Agriculture.

Mirambo

robo (N) 1/4

Lázima ulipe robo ya gharama kwanza. It's necessary that you pay a quarter  
of the amount at the beginning.

Hasani

Kama huna pesa, utapanda nini?

If you don't have money, what will  
you plant?Mirambo

Nitapanda njugu karanga.

I will plant groundnuts.

Notes

A. The MU, KU and PA locative concords.

shambani mwako on ('in') your farm

The mw- prefix belongs to the mu- class of locatives (cf. Unit 29, Note A). A general first-approximation translation equivalent for this class is 'in'. For the ku- class of locatives, whose first-approximation equivalent is 'to', the prefix used with possessive stems is kw-, and for the pa- locatives, it is p-.

The corresponding subject prefixes used with verbs are m-/mw-, ku-/kw-, pa-/p-.

2.

A. Lázima plus subjunctive.

kutumia	Lázima utumie mbolea kwa vitunguu.	You must use fertilizer for onions.
kuagiza	Lázima uagize mbolea kutoka Idara ya Ukulima.	You must order fertilizer from the Agriculture Department.
kulipa	Lázima ulipe robo ya gharama kwanza.	You must pay a quarter of the expenses at first.
kumaliza	Lázima umalize kazi yako kesho.	You must finish your work tomorrow.

B. Relative of the na-tense.

kutumia	Wakulima wanaotumia mbolea watapata vitunguu.	The farmers who use fertilizer will get onions.
---------	---	---

kuagiza	Wakulima wanaoagiza mbolea wataipata.	The farmers who order fertilizer will get it.
kutaka	Wakulima wanaotaka mbolea watalipa robo ya gharama.	The farmers who want fertilizer will pay a quarter of the expense.

## C. MU locative concord with a possessive stem.

muhogo	Twapanda muhogo mwingi shambani mwetu.	We plant a lot of cassava in our garden.
mimea	Twapanda mimea mingi shambani mwetu.	We plant a lot of crops in our garden.
mpunga	Twapanda mpunga mwingi shambani mwetu.	We plant a lot of rice in our garden.
vitunguu	Twapanda vitunguu vingi shambani mwetu.	We plant a lot of onions in our garden.

## D. KU locative concord with a possessive stem.

muhogo	Walileta muhogo mwingi shambani kwetu.	They brought a lot of cassava to our garden.
mimea	Walileta mimea mingi shambani kwetu.	They brought a lot of crops to our garden.
mpunga	Walileta mpunga mwingi shambani kwetu.	They brought a lot of rice to our garden.
vitu	Walileta vitu vingi shambani kwetu.	They brought a lot of things to our garden.

## E. MU and KU locative concords as subject prefixes.

↓	Sandukuni mna chumvi.	There is salt in the box.
soko	Sokoni kuna chumvi.	There is salt at the market.
visu	Sokoni kuna visu.	There are knives at the market.
sanduku	Sandukuni mna visu.	There are knives in the box.

## 3.

## A. MU locative concord with possessive stem and subject prefix.

taa	Nyumbani mwako mna taa? Ndiyo, mna mbili.	Is there a lamp in your house? Yes, there are two.
meza	Nyumbani mwako mna meza? Ndiyo, mna mbili.	Is there a table in your house? Yes, there are two.
saa	Nyumbani mwako mna saa? Ndiyo, mna mbili.	Is there a clock in your house? Yes, there are two.
wino	Nyumbani mwako mna wino? Ndiyo, mna chupa mbili.	Is there ink in your house? Yes, there are two bottles of ink.

## B. KU locative concord with possessive stem and subject prefix.

baiskeli	Nyumbani kwako kuna baiskeli? Ndiyo, kuna moja.	Is there a bicycle at your house? Yes, there is one.
motokaa	Nyumbani kwako kuna motakaa? Ndiyo, kuna moja.	Is there a car at your house? Yes, there is one.
mgonjwa	Nyumbani kwako kuna mgonjwa? Ndiyo, kuna mmoja.	Is there a patient at your house? Yes, there is one.

Conversation Starters

1. A and B are from different parts of Africa (or the United States).

A asks B about what things are like where he is from (kwako).

Unit 73

## 1. Basic Dialogue. Should I get a crop loan?

Hasani

-kopa

to borrow

mahali (PA)

place

Ukitaka, nitakuonyesha mahali pa  
kukopa pesa.

If you like, I'll show you a place to  
borrow money.

Mirambo

moyo (MI)

heart

Sina moyo wa kukopa pesa.

I've no liking for borrowing money.

desturi (N)

a custom, practice

Hii ni desturi mbaya.

It's a bad practice.

Hasani

mwisho (MI)

end

Hivyo ndivyo nilivyofanya, na (or:  
nami) nitazilipa mwisho wa mwaka.

That's how I did, and I will pay it  
[back] the end of the year.

Mirambo

Unajua je kama utapata mavuno mazuri?

How do you know whether you will get  
good crops?

Hasani

wasiwasi (U)

doubt

-angalia

look at

jibu (MA)

answer, reply



Sina wasiwasi. Ukiangalia shambani, I don't have any doubts. If you look  
 utapata majibu. at the farm, you will get the  
 answer.

### Notes

A. Relative affixes in agreement with the objects of verbs.

kiti ulicholeta (or: ...ulichokileta) the chair that you brought  
 karanga tutakazopanda the groundnuts that we will plant  
 (or: tutakazozipanda)

The relative affix (-cho- and -zo- in these examples) may stand for the object of a verb, instead of for its subject. Where it stands for the subject, it must be of the same class as the subject prefix:

(mtu) aliyesikia a person who heard ...

Where it stands for the object, it is in the class of the object:

(kitu) alichomunua (the thing) which he bought...

(motokaa) aliyosikia (the car) which he heard...

The relative affix may then be followed by the object prefix, though many speakers omit the latter.

B. Ndi- plus relative affix.

Ndicho. That is the one (e.g. kitu, kiti, kisu)

Ndiyo. That is the one (e.g. ñchi, motokaa, ndizi)

Ndizo. Those are the ones (e.g. ndizi, nyumba)

Ndivyo. Those are the ones (e.g. vitunguu, vitu)

A combination of ndi- plus the relative affix is translated approximately as in these examples.

C. Combination of the constructions described in Notes A and B.

Ndiye niliyemwona. He is the one I saw.

Ndicho ninachotumia. That is the one (e.g. the thing) that

(or: ...ninachokitumia.) I am using.

The constructions of Notes A and B are combined as shown above.

## D. Concords of VI (plu.) class in expression of manner.

Hivyo ndivyo nilivyofanya. That is how I did.

The concords of the plural VI class are used without antecedent to refer to manner. Compare the use of these same concords in the 'adverbial' forms vizuri, vyema.

## 2.

A. Moyo wa plus infinitive.

kukopa	Sina moyo wa kukopa pesa.	I have no desire to borrow money.
kuendelea	Sina moyo wa kuendelea na masomo.	I have no desire to continue with studies.
kujaribu	Sina moyo wa kujaribu tena.	I have no desire to try again.
kuenda	Sina moyo wa kuenda kwa tabibu.	I have no desire to go to a doctor.

## B. VI plu. concords in expression of manner.

kufanya	Hivyo ndivyo nilivyofanya.	That's how I did it.
kusema	Hivyo ndivyo nilivyosema.	That's how I said it.
kufikiri	Hivyo ndivyo nilivyofikiri.	That's how I thought.
kuja	Hivyo ndivyo nilivyokuja.	That's how I came.
kuanza	Hivyo ndivyo nilivyoanza.	That's how I started.

## C.

kufanya	Nataka kufanya kama ulivyofanya.	I want to do as you did.
kusema	Nataka kusema kama ulivyosema.	I want to speak as you spoke.
kuanza	Nataka kuanza kama ulivyoanza.	I want to start as you started.



kinywaji

4. vyakula Uliagiza vyakula vizuri? Did you order good food?  
 Ndiyo. Vyakula nilivyoviagiza Yes, the food that I  
 vilikuwa vizuri sana. ordered is very good.

viberiti

5. mikate Uliagiza mikate mizuri? Did you order some good  
 loaves?  
 Ndiyo. Mikate niliyoiagiza Yes, the loaves that I  
 ilikuwa mizuri sana. ordered are very good.

mimea

Unit 74

## 1. Basic Dialogue. Farm implements.

Hasani

-lima

to cultivate

kwenu

at your place

Je, kwenu mwatumia vyombo gani kwa  
kulimia?

Say, what tools do you use in farm-  
ing where you live?

Mirambo

jembe (MA)

hoe

uma (U, N)

rake

Tunatumia majembe na nyuma.

We use hoes and rakes.

Hasani

Kuna wakulima wanaotumia plau?

Are there farmers who use plows?

Mirambo

Ndiyo, wale walio na mashamba  
makubwa.

Yes, those who have large farms.

Hasani

mti (MI)

tree

kijiti (VI)

small tree, underbrush

-kata

to cut

Mkisha angusha miti mnakata vijiti  
na nini?

When you have finished felling trees,  
what do you cut the brush with?

Mirambo

panga (MA)

large knife

Wengi hukata vijiti kwa mapanga.

Many cut the brush with pangas.

Hasani

laini

soft, smooth

Na kwa kulainisha udongo?

And for softening the ground?

(or: na kwa kutifua udongo?)

Mirambo

Panga latosha.

A panga is all right.

Notes

A. Locative concord plus possessive stem, with no antecedent.

Kwetu tunatumia majembe. At our place, we use hoes.

The concord kw- plus possessive stem is used where English would have 'at your place', 'where we live', etc.

B. The spelling of -ki(i)sha.

The forms which in Standard Swahili are spelled akiisha, nikiisha, etc. are commonly pronounced with only one i.

2.

A. Concords with mahali.

~ema	Tumeona mahali pema leo.	We have found a good place today.
~ngapi	Tumeona mahali pangapi leo?	How many places have we found today?
kupanda	Tumeona mahali pazuri pa kupanda muhogo leo.	We have found a good place for planting cassava today.
kuogelea	Tumeona mahali pazuri pa kuogelea leo.	We have found a good place for swimming today.

B.

kuweka	Wapi mahali pa kuwekea taa?	Where does the lamp belong?
--------	--------------------------------	-----------------------------

kupata	Wapi mahali pa kupatia dawa?	Where is the place to get medicine?
kununua	Wapi mahali pa kununua pombe?	Where is the place to buy beer?
kuvaa	Wari mahali pa kuvaa nguo?	Where is the dressing room?

C. -kisha plus verb stem.

kuangusha	Ukisha angusha miti hii, rudi nyumbani.	When you finish felling these trees, return home.
kulainisha	Ukisha lainisha udongo huu, rudi nyumbani.	When you finish breaking up the earth, return home.
kufuta	Ukisha futa maji haya, rudi nyumbani.	When you finish wiping up the water, return home.
kusafisha	Ukisha safisha majembe haya, rudi nyumbani.	When you finish cleaning these hoes, return home.
kupigwa	Ukisha pigwa sindano, rudi nyumbani.	When you finish getting your injection, return home.

3.

A. Na-tense: indicative vs. relative.

kutumia	Wakulima wengi wanatumia plau? Hapana, wanaotumia plau ni wachache.	Do many farmers use ploughs? No, those who use ploughs are few.
kujua	Watu wengi wanajua kutengeneza motakaa? Hapana, wanaojua kutengeneza motakaa ni wachache.	Do many people know how to repair cars? No, those who know how to repair cars are few.

<p>kuangusha    Watu wengi wanaangusha miti                   kwa visu?                   Hapana, wanaoangusha miti                   kwa visu ni wachache.</p>	<p>Do many people fell trees with knives? No, those who fell trees with knives are few.</p>
<p>kuhudhuria    Wanafunzi wengi wanahudhuria                   vyuo vya juu?                   Hapana, wanaohudhuria vyuo                   vya juu ni wachache.</p>	<p>Do many students attend universities? No, those who attend universities are few.</p>
<p>B. Relative counterpart of <u>a</u>-tense.</p>	
<p>majembe      Wako wapi wanaume walio na                   majembe?                   Wale walio na majembe                   wamekwisha kwenda shambani.</p>	<p>Where are the men with hoes?  Those who have hoes have already gone to the garden.</p>
<p>uma            mapanga</p>	



Unit 75

## 1. Basic Dialogue. Times for planting and weeding.

Hasani

mbegu (N)

seed

Utapanda mbegu zako lini?

When are you going to plant your seeds?

MiramboMvua ikinyesha nitazipanda mbegu  
zangu.

I'll plant them when it rains.

Hasani

-palilia

to weed

Umenunua vyombo vya kupalilia?

Have you bought the tools for weeding?

Mirambo

kitambo

a short period of time,  
a piece (of time)Kitambo! Mapanga sita na majembe  
matano.

Long ago! Six pangas and five hoes.

HasaniLakini, ni wakati gani mzuri wa  
kupalilia?But what time is a good one for  
weeding?MiramboTuseme, kama mimea ikisha pata inchi  
sita hivi.Let's say, when the plants have already  
gotten [to] about six inches.Hasani

-mea

to grow

-ota

to shoot out

jani (MA)

leaf

Maana yake ikisha ota majani?

That is to say, when they put out  
[their] leaves?Mirambo

Ndiyo.

Yes.

2.

A. wakati wa plus infinitive.kupanda Wakati gani mzuri wa  
kupanda mbegu?When is the best time to plant  
seeds?kupalilia Wakati gani mzuri wa  
kupalilia shamba?When is the best time to weed a  
garden?kukata Wakati gani mzuri wa  
kukata vijiti

When is the best time to cut brush?

kulainisha Wakati gani mzuri wa  
kulainisha udongo?When is the best time to break up  
the soil?

3.

A. Me-tense (affirmative) vs. -ja- negative.kupalilia Umepalilia mahindi yako?  
Bado sijapalilia.Have you weeded your maize?  
Not yet, I haven't.kupanda Umepanda muhogo wako?  
Bado sijapanda.Have you planted your cassava?  
Not yet, I haven't.kupeleka Umepeleka kalamu yako kwa  
fundu?  
Bado sijapeleka.Have you taken your pen to the  
repairman?  
Not yet, I haven't.

## B.

kuvuna	Wakulima wamevuna mtama? Hapana. Bado hawajavuna.	Have the farmers harvested millet? - No, they haven't yet.
kupanda	Wakulima wamepanda mtama? Hapana. Bado hawajapanda.	Have the farmers planted millet? No, they haven't yet.
kutenge- neza	Fundi ametengeneza kalamu yako? Hapana. Bado hajatengeneza.	Has the pen repairer repaired your pen? No, he hasn't yet.

C. Infinitive vs. affirmative subjunctive vs. negative subjunctive.

mpunga	M̄punga huo unahitaji kupaliliwa. Tuupalilie kesho. Tusiupalilie leo.	That rice requires weeding.  Let's weed it tomorrow. Let's not weed it today.
mtama	M̄tama huo unahitaji kupaliliwa. Tuupalilie kesho. Tusiupalilie leo.	That millet requires weeding.  Let's weed it tomorrow. Let's not weed it today.
mahindi	Mahinci haya yanahitaji kupaliliwa. Tuyapalilie kesho. Tusiyapalilie leo.	This maize requires weeding.  Let's weed it tomorrow. Let's not weed it today.
maharagwe	Maharagwe haya yanahitaji kupaliliwa. Tuyapalilie kesho. Tusiyapalilie leo.	These beans require weeding.  Let's weed them tomorrow. Let's not weed them today.
njugu	Njugu hizi zinahitaji kupaliliwa. Tuzipalilie kesho. Tusizipalilie leo.	These groundnuts require weeding.  Let's weed them tomorrow. Let's not weed them today.

muhogo Muhogo huo unahitaji  
kupaliliwa.

Tuupalilie kesho.

Tusiupalilie leo.

This cassava requires weeding.

Let's weed it tomorrow.

Let's not weed it today.

Conversation Starters

1. Discuss agricultural practices in the part of Africa in which you are most interested.

Unit 76

## 1. Basic Dialogue. Boy or Girl?

Hadija

Bibiye amepata mtoto wa kiume au wa kike? Did his wife have a boy or a girl?

Hamisi

Mtoto wa kiume. A boy.

Hadija

Je, hawajambo? Are they all right?

Hamisi

mgongo (MI) back

Hawajambo, lakini mama aumwa mgongo. They're all right, but the mother's back is hurting her.

Hadija

kujifungua to release oneself

Pengine ni kwa sababu ya kujifungua. Maybe it's because of delivering the baby.

Hamisi

nafuu (N) advantage

Atapata nafuu tu. She'll recover.

Hadija

Mtoto mwenyewe ana matata? How is the baby himself?

Hamisi

fujo (MA) disturbance

wala	nor, neither
matata (pl. MA)	complications
Mzuri sana. Hana fujo wala matata.	Very fine. He has no trouble or complications.

### Notes

#### A. Wala between negatives.

Wala either is both preceded and followed by a negative verb, or it joins two nouns which are in parallel relation to the same negative verb. See the exercises for further examples.

2.

#### A. Some special forms for possessives with family relationships.

mke	Mkeo anapata nafuu?	Is your wife recovering?
hibi	Bibi yako anapata nafuu?	Is your wife recovering?
mtoto	Mtoto wako anapata nafuu?	Is your child recovering?
baba	Baba yako anapata nafuu?	Is your father recovering?
mama	Mama yako anapata nafuu?	Is your mother recovering?
mume	Mumeo anapata nafuu? (or: Bwana wako...)	Is your husband recovering?
ndugu	Nduguyo anapata nafuu?	Is your brother recovering?
dada	Dadio anapata nafuu? (or: Dada yako...)	Is your sister recovering?

#### B. Wala

taa	Sina taa wala mafuta.	I have neither lamp nor oil.
chai	Sina chai wala kahawa.	I have neither tea nor coffee.
baiskeli	Sina baiskeli wala motakaa.	I have neither bicycle nor automobile.

## C.

kiti	Wanafunzi hawana viti wala meza.	The students have neither chairs nor tables.
kitabu	Wanafunzi hawana vitabu wala kalamu.	The students have neither books nor pens.
mwalimu	Wanafunzi hawana mwalimu wala shule.	The students have neither teacher nor school.

## D.

kusoma	Wanaume hawa hawajui kusoma wala kuandika.	These men know neither reading nor writing.
Kiingereza	Wanaume hawa hawajui Kiingereza wala Kiswahili.	These men know neither English nor Swahili.

## 3.

## A. Concords, including relative forms of verbs.

kitabu	Nilinunua kitabu juzi.  Kitabu nilichonunua juzi ni kibaya. (or: ...nilichokinunua...)	I bought a book the day before yesterday.  The book which I bought the day before yesterday is bad.
baiskeli	Nilinunua baiskeli juzi.  Baiskeli niliyonunua juzi ni mbaya.	I bought a bicycle the day before yesterday.  The bicycle which I bought the day before yesterday is bad.
visu	Nilinunua visu juzi.  Visu nilivyonunua juzi ni vibaya.	I bought knives the day before yesterday.  The knives which I bought the day before yesterday are bad.

mafuta	<p>Nilinunua mafuta juzi.</p> <p>Mafuta niliyonunua juzi ni mabaya.</p>	<p>I bought oil the day before yesterday.</p> <p>The oil which I bought the day before yesterday is bad.</p>
jembe	<p>Nilinunua jembe juzi.</p> <p>Jembe nililonunua juzi ni baya.</p>	<p>I bought a hoe the day before yesterday.</p> <p>The hoe which I bought the day before yesterday is bad.</p>
nanasi	<p>Nilinunua nanasi juzi.</p> <p>Nanasi nililonunua juzi ni baya.</p>	<p>I bought a pineapple the day before yesterday.</p> <p>The pineapple which I bought the day before yesterday is bad.</p>
ndizi	<p>Nilinunua ndizi juzi.</p> <p>Ndizi nilizonunua juzi ni mbaya.</p>	<p>I bought bananas the day before yesterday.</p> <p>The bananas which I bought the day before yesterday are bad.</p>
wino	<p>Nilinunua wino juzi.</p> <p>Wino nilionunua juzi ni mbaya.</p>	<p>I bought some ink the day before yesterday.</p> <p>The ink which I bought the day before yesterday is bad.</p>
taa	<p>vitunguu      maharagwe</p>	



Unit 77

## 1. Basic Dialogue. Prenatal care.

Mirambo

mja mzito

a pregnant person

-tunza

to care for

Mama mja mzito hutunzwaje?

How is a pregnant woman cared for?

MohamedHupelakwa hospitalini akiwa karibu  
kujifungua.She is taken to the hospital when she  
is about to deliver.Mirambo

Mle anafanya nini?

What does she do in there?

Mohamed

-pima

to measure, examine

Bwana daktari humpima na kumpa  
dawa.The doctor examines her and gives her  
medicine.

-lisha

to feed ('cause to eat')

Pia humpa chakula cha kumlisha  
mtoto.She is also given food for nourishing  
the child.Mirambo

tunzo (MA)

care

Wanapata matunzo safi?

Do they get good care?

Mohamed

-punzika

to rest

Sana, hata mapunziko.

Very much so. [They] even [get a lot  
of] rest.

NotesA. Sequence of verbs joined by na.

daktari humpima na kumpa dawa    the doctor examines her and gives  
her medicine

Here, the single subject word daktari is followed by two verbs, the stems of which are -pima and -pa. Where the action of the second verb is not clearly the goal or result of the action of the first, the second is in the infinitive form, following na 'and'.

2.

A. Causative stems based on -la and -nywa.

	Usi <u>l</u> ishe mtoto!	Don't feed the child!
↓		
kunyw <u>e</u> sha	Usi <u>nyw</u> eshe mtoto!	Don't give the child anything to drink!
watoto	Usi <u>w</u> anyweshe watoto!	Don't give the children anything to drink!
kul <u>i</u> sha	Usi <u>w</u> alishe watoto!	Don't feed the children!

B. Subjunctive with -ka- after -enda.

kuk <u>a</u>	Kaa kitako upum <u>z</u> ike.	Sit down and rest.
kw <u>e</u> nda	Nenda nyumbani ukapum <u>z</u> ike.	Go home and rest.
ku <u>ing</u> ia	Ingia nyumbani upum <u>z</u> ike.	Get into the house and rest.

C. Passive stem based on -pa.

kalamu	Wanafunzi walipewa kalamu zao.	The pupils were given their pens.
vitabu	Wanafunzi walipewa vitabu vyao.	The pupils were given their books.
viti	Wanafunzi walipewa viti vyao.	The pupils were given their chairs.

meza	Wanafunzi walipewa meza zao.	The pupils were given their tables.
D. <u>-tunza.</u>		
watoto	Kazi yangu ilikuwa kutunza watoto.	My job was to care for children.
ng'ombe	Kazi yangu ilikuwa kutunza ng'ombe.	My job was to care for cows.
nguruwe	Kazi yangu ilikuwa kutunza nguruwe.	My job was to care for pigs.
taa zetu zote	Kazi yangu ilikuwa kutunza taa zetu zote.	My job was to care for all our lamps.

## 3.

A. MU and KU locative concords with subject prefixes and demonstratives.

hospitali	Hospitalini mnafanywa nini? Mle wagonjwa wanatunzwa.	What is done in the hospital? There patients are cared for.
shule	Shuleni mnafanywa nini? Mle wanafunzi wanasomesywa.	What is done in the school? There pupils are taught.
soko	Sokoni kunafanywa nini? Kule vyakula vinauzwa.	What is done at the market? There (foodstuffs) are sold.
pwani	Pwani kunafanywa nini? Kule watu wanaogelea.	What is done at the beach? There people swim.

Unit 78

## 1. Basic Dialogue. Post-natal care. (cont'd from Unit 77)

Mirambo

Wakiisha kuzaa wanakaa hospitalini? When they have finished delivering,  
do they stay in the hospital?

Mohamed

Ndiyo, kwa siku chache tu. Yes, for just a few days.

Mirambo

-lia to cry  
Mtoto akilia, hupewa chakula? When the baby cries, is it given food?

Mohamed

~changa young  
-nyonya to suck  
Akiwa mchanga sana, mama If it is very young, the mother nurses  
humi nyonyesha. it.

Mirambo

hasa exactly, very much  
Hasa, ni chakula gani watoto Just what food do babies like?  
hupenda?

Mohamed

Kwa kawaida, maziwa. In general, milk.

Mirambo

-beba to carry a child on back or hip  
Kwenu mama hubeba watoto? At your place does the mother carry  
the children on her back?

Mohamed

mbavuni

by the ribs

mbeleko (N)

cloth or sling for carrying  
a child

Ndiyo, huwabeba mgongoni, au  
mbavuni katika mbeleko.

Yes, they carry them on [their]  
back[s] or on [their] hip[s] in  
a sling.

2.

A. -lilia.

nini? Mtoto analilia nini?

What is the child crying for?

chakula Mtoto analilia chakula.

The child is crying for food.

maziwa Mtoto analilia maziwa.

The child is crying for milk.

mama Mtoto analilia mama.

The child is crying for the mother.

chai baba sukari Hamisi

## B. Negative imperative.

kuliza Usimlize mtoto!

Don't make the child cry.

kunyo- Usimnyonyeshe mtoto.  
nyesha

Don't nurse the child.

kulisha Usimlishe mtoto.

Don't feed the child.

kupa Usimpe mtoto kisu!

Don't give the child a knife.

## C. KU locative: concords with various possessive stems.

ninyi Kwenu wapi?

Where is your (pl.) home?

wewe Kwako wapi?

Where is your (sg.) home?

yeye Kwake wapi?

Where is his/her home?

wao Kwao wapi?

Where is their home?

## D. PA locative concord with various possessive stems.

sisi	Hapa petu.	This is our home.
mimi	Hapa pangu.	This is my home.
wao	Hapa pao.	This is their home.
yeye	Hapa pake.	This is his home.

## 3.

A. -kwisha plus verb stem vs. negative imperative.

kulisha	Usimlishe mtoto! Amekwisha lishwa na dada yake.	Don't feed the child! It has already been fed by its sister.
kuryweshwa	Usimnyonyeshe mtoto! Amekwisha nyonyeshwa na mama yake.	Don't nurse the child! It has already been nursed by its mother.
kuliza	Usimlize mtoto! Amekwisha lizwa.	Don't make the child cry! It has already been made to cry.
kupa chakula	Usimpe mtoto chakula. Amekwisha pewa na mama yake.	Don't give the child food! It has already been given food by its mother.

Conversation Starters

1. A and B compare notes on the problems of pre- and post-natal care in Africa and in the United States.

Unit 79

1. Basic Dialogue. When are you getting married?

Magese

-oa

to marry

Utaca lini, Ochieng?

When are you going to get married

Ochieng?

Ochieng

mchumba

boy/girl friend, fiancé(e)

Wakati mchumba wangu atakaporudi.

At the time when my fiancée returns.

Magese

Kwani yuko wapi?

Oh? Where is she?

OchiengAlikwenda kusomesha huko upande  
wa Kisumu.She went to teach in the region of  
Kisumu.Magese

mahari

lobola, dowry

Umelipa mahari au bado?

Have you paid the dowry or not (yet)?

Ochieng

-ngoja

to wait

Bado. Namngoja arudi.

Not yet. I'm waiting for her to  
return.Magese

-kubali

to agree

Wazazi wako na wake wamekubali?

Have your parents and hers given their  
consent?

Ochieng-zua

to prevent

Hawawezi kunizua nisisimwoe.

They can't prevent me from marrying  
her.NotesA. Relative future forms with -taka-.

The future tense in its non-relative forms uses -ta- as its tense prefix, but in relative forms uses the disyllabic prefix -taka-.

B. Two verbs that are followed by subjunctive forms.

Note that subjunctive verb forms often follow the verbs -zua 'to prevent from' and -ngoja 'to wait'. The former is followed by the negative subjunctive.

2.

A. -zua plus negative subjunctive.

kusema	Huwezi kunizua nisiseme.	You can't prevent me from talking.
kwenda	Huwezi kunizua nisiende.	You can't prevent me from going.
kulewa	Huwezi kunizua nisilewe.	You can't prevent me from being drunk.
kurudi	Huwezi kunizua nisirudi.	You can't prevent me from coming back.
kuendelea	Huwezi kunizua nisiendele.	You can't prevent me from moving on.

B.

kusema	Hamwezi kuwazua wasiseme.	You can't prevent them from talking.
kula	Hamwezi kuwazua wasile.	You can't prevent them from eating.



kuelewa      kujifunza      kusikitika

C.

kuona      Hatuwezi kuwazuia wasimwone.      We can't prevent them from seeing him.

kusaidia      Hatuwezi kuwazuia wasimsaidie.      We can't prevent them from helping him.

kusikia      kupenda      kupiga

D. -ngoja plus subjunctive.

kusema      Hatutakungoja useme.      We'll not wait for you to speak.

kwanza      Hatutakungoja uanze.      We'll not wait for you to begin.

kwenda      kujitayarisha      kurudi

E. Verb phrase with -wa.

kusema      Ali alikuwa akingoja niseme.      Ali was waiting for me to speak.

kuja      Ali alikuwa akingoja ni je.      Ali was waiting for me to come.

kufuata      kutangulia      kumaliza      kuingia

3.

A. -ja- negative vs. affirmative subjunctive.

Bado hajasema.      He hasn't spoken yet.

Tutangoja aseme.      We'll wait for him to speak.

Bado sijasema.      I haven't spoken yet.

Tutakungoja useme.      We'll wait for you to speak.

Bado hawajasema.      They haven't spoken yet.

Tutawangoja waseme.      We'll wait for them to speak.

Bado hajaenda.      He hasn't gone yet.

Tutangoja aende.      We'll wait for him to go.

B. Infinitive vs. negative subjunctive.

kisu	Nataka kukinunua kisu hiki. Usijaribu kunizuia nisikinunue.	I want to buy this knife. Don't try to prevent me from buying it.				
vitabu	Nataka kuvinunua vitabu hivi. Usijaribu kunizuia nisivinunue.	I want to buy these books. Don't try to prevent me from buying them.				
mbegu	Nataka kuzinunua mbegu hizi. Usijaribu kunizuia nisizinunue.	I want to buy these seeds. Don't try to prevent me from buying it.				
sanduku	ng'ombe	nguruwe	mkate	mikate	imea	imea

Unit 80

1. Basic Dialogue. Come along to the wedding!

Ochieng

wiki (N)

week

Je, ndugu yangu, wajua kwamba nitaoa

Say, brother, do you know I'm going

wiki ijayo?

to get married next week?

Magese

Kweli? Hiyo sijasikia bado.

Really? I hadn't heard (yet).

harusi (N) (or: arusi)

wedding

Harusi itakuwa siku gani?

What day will the wedding be?

Ochieng

kutwa

to set (of the sun)

Kesho kutwa, bwana.

The day after tomorrow.

Magese

-unga

to join

(-ungana)

to join one another

Nani atakayewaunganisheni?

Who is going to marry you?

('...to cause you to join one another')

Ochieng

kasisi (MA pers.)

clergyman, priest

Kasisi Kamau.

The Reverend Mr. Kamau.

Magese

-fika

to arrive

-shangilia	to make rejoicings for
Nitafika kuwashangilieni.	I'll be there to cheer for you.
-simama	to stand up
Nani ambao watawasimamieni?	Who will stand up with you?

Ochieng

mume (pl. waume)	husband
Dada yangu na mumewe.	My sister and her husband.

NotesA. Relative phrases with amba-.

Certain tenses do not take the relative affix at all. Instead they form relative phrases in the following manner:

amba, plus rel. affix, plus indicative verb

vitabu ambavyo hujaviuza      the books that you haven't sold yet

Even tenses which may take the relative affix sometimes form relative phrases in this way. See the exercises for further examples.

## B. Object affix(es) for second person plural.

The object pronouns for first and third person singular and plural, and for second person singular, are simple in form and are used all over the Swahili speaking area. The second person plural object prefix is different in both ways: it is variously represented in different forms of Swahili (see Ashton, p. 42 for details); it also involves both a prefixial element (identical with the 3 plu. or 2 sg. object prefix) and a suffixed element. For examples of one variant, see the exercises.

## 2.

## A. Second person plural object.

kupa	Haruna hataki kuwapeni kalamu	Haruna does not want to give
	zenu.	your pens to you.

**kuletea** Haruna hataki kuwaleteeni  
kalamu zenu. Haruna does not want to bring  
your pens to you.

kuonyesha kupatia kutengenezea kurudishia

B. Relative forms with amba- -o.

**kusoma** Nitavisoma vitabu ambavyo  
sijaviuza. I'll read the books which I  
haven't sold.

**kuleta** Nitavileta vitabu ambavyo  
sijaviuza. I'll bring the books which I  
haven't sold.

**kupa** Nitakupa vitabu ambavyo  
sijaviuza. I'll give you the books which  
I haven't sold.

**kuonyesha** Nitavionyesha vitabu  
ambavyo sijaviuza. I'll show the books which I  
haven't sold.

C.

**vitabu** Nenda ukavichukue vitabu  
ambavyo hujaviuza. Go and get the books which you  
haven't sold.

**vitu** Nenda ukavichukue vitu  
ambavyo hujaviuza. Go and get the things which you  
haven't sold.

**wino** Nenda ukauchukue wino  
ambao hujauza. Go and get the ink which you  
haven't sold.

**kalamu** Nenda ukaichukue kalamu  
ambayo hujaiuza. Go and get the pen which you  
haven't sold.

**jembe** Nenda ukalichukue jembe  
ambalo hujaliuza. Go and get the hoe which you  
haven't sold.

**mazao** Nenda ukayachukue mazao  
ambayo hujayauza. Go and get the crops which you  
haven't sold.

**mkate** Nenda ukauchukue mkate  
ambao hujauza. Go and get the loaf of bread  
which you haven't sold.

mimea	Nenda ukaichukue mimea ambayo hujaiuza.	Go and get the plants which you haven't sold.
-------	--	--

3.

A.

vikombe	Nimeleta vikombe. Vikombe ambavyo umeleta ni vingapi?	I have brought cups. ( 'The cups which you have brought, how many are they?' )
visahani	Nimeleta visahani. Visahani ambavyo umeleta ni vingapi?	I have brought saucers. How many saucers have you brought?

kalamu      sindano      majembe      mikate      mimea      wapagazi  
wanafunzi

### Conversation Starters

1. What kind of woman (man) would you like to marry? (This topic is one which allows ample opportunity for the use of the relative forms of verbs.)

## Reading Selection III

Shule za Tanganyika Zamani.

Nchini Tanganyika mlikuwa shule za namna tatu hasa. Zile zilizoendeshwa na serikali, misheni, na pia wenyeji. Shule hizo zote zilikuwa na madarasa kutoka ya chini kabisa mpaka ya juu. Lakini zile za wenyeji zilifikia madarasa ya katikati tu, kwa sababu baadaye wanafunzi waliingia zile nyingine.

Watoto walianza masomo yao yote katika lugha ya Kiswahili. Hawakujifunza katika lugha za makabila yao. Walipofika darasa la tano, yaani baada ya kusoma kwa muda wa miaka minne, walianza kujifunza Kiingereza. Lugha mbili zilianza kutumiwa. Baadaye masomo yalikuwa katika Kiswahili na Kiingereza; halafu mafunzo yote yalikuwa katika Kiingereza tu mpaka mwanafunzi alipohitimu na kuendelea na masomo ya juu katika chuo kikuu.

Katika shule za chini, watoto walianza kuhudhuria shule walipokuwa na umri wa miaka sita au saba. Lakini sasa wengi huanza kusoma wakiwa na umri wa miaka mitano hivi. Shule nyingi za chini hazikuwa za serikali kwa kawaida. Zamani kidogo watoto wachache walipata nafasi ya kusoma na kuandika, lakini sasa kwa ajili ya juhudi kuu iliyofanywa na wakuu wa Idara ya Elimu watoto wengi wanaelimishwa kila mwaka. Wingi wao unazidi sana mwaka kwa mwaka kwa jinsi ambavyo hata shule za juu zinashindwa kuwapokea wote. Skuli hizo ndogo ndogo, ambazo wakati mwingine ziliitwa 'shule za vijijini' zilikuwa na madarasa ya kwanza manne tu. Mkuu wa walimu waliofundisha humo aliitwa Mwalimu Mkuu, na ndiye aliyesimamia na kuendesha shule za vijijini.

yaani	that is to say	wingi (U)	majority, number
juhudi (N)	effort, exertion	funzo (MA)	(course of) instruction
-elimisha	to educate	<b>zamani</b>	time past
jinsi (N, but often used with concords of VI)	way, manner	-shinda	to overcome
		-pokea	to accept
		-simamia	to oversee, supervise

## Questions and Answers over Reading Selection

QuestionsSample Answers

- |  |   |
|--|---|
| 1. Nchini Tanganyika mlikuwa na shule za namna ngapi?                  | Mlikuwa na shule za namna tatu hasa.                                |
| 2. Shule hizo ni zipi?   | Zile zilizoendeshwa na serikali, misheni, na wenyeji.               |
| 3. Je, shule hizo zilikuwa na madarasa mpaka ya juu?                   | Ndiyo, lakini za wenyeji zilikuwa na madarasa mpaka ya katikati tu. |
| 4. Je, wanafunzi katika shule za wenyeji waliingia zile nyingine?      | Ndiyo, waliingia.   |
| 5. Watoto walianza masomo yao katika lugha za makabila yao?            | Hapana, bwana, mafunzo yote yalikuwa katika Kiswahili.              |
| 6. Je, Kiingereza?   | Kiingereza! Watoto walijifunza walipofika darasa la tano.           |
| 7. Lugha gani zilitumiwa katika mafunzo baada ya kujifunza Kiingereza? | Kiingereza.   |
| 8. Watoto walianza shule wakiwa wakiwa na umri gani?                   | Miaka sita au saba, lakini sasa wengi huwa na miaka mitano hivi.    |
| 9. Skuli zote za chini zilikuwa za serikali?                           | La, nyingine zilikuwa za misheni na za wenyeji.                     |
| 10. Watoto wachache wanapata nafasi ya kusoma na kuandika?             | La, zamani kidogo. Lakini sasa wanaelimishwa wengi mwaka kwa mwaka. |



- 
11. Skuli ndogo ndogo ziliitwaje? Wakati mwingine ziliitwa 'shule za vijijini'.
12. Shule za vijijini zilikuwa na madarasa mengi? Hapana, zilikuwa na madarasa ya kwanza marne tu.
13. Mkuu wa walimu alitwa Mwalimu Mkuu? Ndiyo.
14. Mwalimu Mkuu alisimamia shule za vijijini? Ndiyo, pia aliziendesha.

Review Sentences, Units 1 - 80

- |  |  |
|--|--|
| 1. Juma aliwapatieni pesa ngapi?                     | How much money did Juma get them?                          |
| 2. Watu wengi wa nchi hii hunywa kahawa nyingi.      | Many people of this country drink a lot of coffee.         |
| 3. Unaweza kuitengeneza baiskeli hii?                | Can you fix this bicycle?                                  |
| 4. Siwezi, lakini nitaipeleka kwa fundi.             | I can't, but I'll take it to the repairman.                |
| 5. Maduka mengi huuza nguo na mengine huuza vyakula. | Many shops sell clothes, and others food.                  |
| 6. Afrika ya mashariki ni nchi nzuri sana.           | East Africa is a very beautiful country.                   |
| 7. Wenyeji wa nchi hiyo huongea lugha mbali mbali.   | The natives of that country speak various languages.       |
birika (MA)

pot (tea)

Leta vikombe na visahani vyake,

Bring the cups and saucers, the sugar

bakuli la sukari na birika la chai.

bowl, and the tea pot.

Juma

Ngoja kidogo.

Wait a bit.

Notes

## A. Concord with two or more nouns.

Where two inanimate nouns (e.g. chai and kahawa) are the subject of the same verb, the question arises which subject prefix to use. The question is further complicated when the two nouns happen to belong to different classes (e.g. uma and jembe). Speakers differ in their practice in such situations; a final resolution of the problem must await further study.

B. ake with an inanimate plural antecedent.vikombe na visahani vyake

Hitherto we have translated ake as either 'his' or 'her'. It may also correspond to the English possessive forms its and their(s). Note that ake is the stem used whether the inanimate antecedent of the stem (vikombe in this example) is singular or plural. Contrast, with animate nouns, ake when the antecedent is singular and ao when it is plural:

akulima na watoto wakewakulima na watoto wao

2.

A. Verb phrase with ne-tense in second verb.

siagi Jana tulikuwa tumeishiwa siagi. Yesterday we were short of butter.

chumvi	Jana tulikuwa tumeishiwa chumvi.	Yesterday we were short of salt.
sukari	Jana tulikuwa tumeishiwa sukari.	Yesterday we were short of sugar.
wino	Jana tulikuwa tumeishiwa wino.	Yesterday we were short of ink.
sabuni	Jana tulikuwa tumeishiwa sabuni.	Yesterday we were short of soap.
mafuta	Jana tulikuwa tumeishiwa mafuta.	Yesterday we were short of oil.

B. -ja- negative; -ondoa with locative.

vyombo	Kwa nini hujaondoa vyombo mezani?	Why haven't you removed the utensils from the table?
sahani	Kwa nini hujaondoa sahani mezani?	Why haven't you removed the plates from the table?
vijiko	vikombe	kitambaa

3.

A. Concord: Subject prefix with two noun subjects.

chai	Chai iko tayari.	The tea is ready.
kahawa	Kahawa iko tayari.	The coffee is ready.
	Chai na kahawa viko (or: iko) tayari.	The tea and coffee are ready.
bilauri	Bilauri ziko tayari.	The glasses are ready.
sahani	Sahani ziko tayari.	The plates are ready.
	Bilauri na sahani ziko (or: viko tayari) tayari.	The glasses and plates are ready.

B.

suruali (sg.)	Suruali iko tayari.	The trousers are ready.
------------------	---------------------	-------------------------

koti	Koti liko tayari.	The coat is ready.
uma	Uma uko (or: iko) tayari.	The fork is ready.
suruali (pl.)	Suruali ziko tayari.	The trousers are ready.
makoti	Makoti yako tayari.	The coats are ready.
suruali na makoti	Suruali na makoti viko (or: yako) tayari.	The trousers and coats are ready.
kalamu (pl.)	Kalamu ziko tayari.	The pens are ready.
wino	Wino uko tayari.	The ink is ready.
kitanda	Kitanda kiko tayari.	The bed is ready.
bakuli	Bakuli liko tayari.	The bowl is ready.
birika	Birika liko (or: iko) tayari.	The kettle is ready.
vyakula	Vyakula viko tayari.	The food is ready.
kalamu na wino	Kalamu na wino viko (or: upo) tayari.	The pens and ink are ready.

Unit 97

## 1. Basic Dialogue. Washing dishes.

Hadija

Nani atakayesafisha vyombo leo?

Who is going to wash the dishes  
today?Juma

Mimi, mama, Asha atanisaidia.

I [will], mother. Asha will help me.

Hadija

Nitawapatieni maji ya moto.

I'll get you some hot water.

JumaAsha, tafadhali lete sabuni na  
vitamba.

Asha, please bring soap and cloths.

Hadija

ili

so that

-chelesha

to boil

Nimechelesha maji ili yaondoe mafuta  
katika vyombo.I've boiled the water so that it will  
remove the grease from (on) the  
plates.Juma

Asante, mama.

Thank you, Mother.

Hadija

kabati (N or MA)

cupboard

Asha, weka vyombo vilivyokauka  
kabatini.Asha, put the dry plates in the cup-  
board.

Junna

-ng'ang'ania

here: to stick to

Mayai yameng'ang'ania katika sahani.      Some egg is stuck to the plate.

Hadija

Irudishe majini ili uisafishe

Put it back into the water so that

visuri.

you [can] get it good and clean.

NotesA. The subjunctive with ili.Note the use of the subjunctive after ili 'so that'.

2.

A. Relative and locative suffixes on the same verb.

vyombo      Vyombo vilivyomo kabatini  
vimekauka.

The utensils that are in the  
cupboard are dry.

vikombe

sahani      Sahani zilizomo kabatini  
zimekauka.

The plates that are in the cup-  
board are dry.

bilauri      nguo      kisu      kijiko

uma      nyuma

B.

vyombo      Vyombo vilivyoko mezani  
vina majimaji.

The utensils that are on the  
table are wet.

visahani

sahani      Sahani zilizoko mezani  
zina majimaji.

The plates that are on the table  
are wet.

nguo      kisu      kijiko      uma      nyuma

## C. Concord: noun object in first clause and subject prefix in second.

vyombo	Weka vyombo mezani ili vikauke.	Put the utensils on the table to dry.
nyuma	Weka nyuma mezani ili zikauke.	Put the forks on the table to dry.
bilauri	Weka bilauri mezani ili zikauke.	Put the glasses on the table to dry.
uma	Weka uma mezani ili ikauke.	Put the fork on the table to dry.

## 3.

A. -na-tense affirmative vs. -ja- negative.

maji	Maji yanachemka? Hapana, hayajachemka bado.	Is the water boiling? No. It hasn't boiled yet.
chai	Chai inachemka? Hapana, haijachemka bado.	Is the tea boiling? No. It hasn't boiled yet.
kahawa	Kahawa inachemka? Hapana, haijachemka bado.	Is the coffee boiling? No. It hasn't boiled yet.
maziwa	Maziwa yanachemka? Hapana, hayajachemka bado.	Is the milk boiling? No. It hasn't boiled yet.

## B. Concord in multiple positions.

viazi	Viazi hivi havina moto. Virudishe ndani ya jiko ili vipate moto.	These potatoes are not warm. Put them back on the fire to get warm.
nyama	Nyama hii haina moto. Irudishe ndani ya jiko ili ipate moto.	This meat is not warm. Put it back in the kitchen to get warm.
mboga	Mboga hizi hazina moto. Zirudishe ndani ya jiko ili zipate moto.	These vegetables are not warm. Put them back on the fire to get warm.

wali Wali huu hauna moto.

This rice is not warm.

Urudishe ndani ya jiko ili  
upate moto.

Put it back on the fire to get  
warm.

### Conversation Starters

1. A (a mother) discusses with B (a domestic servant) B's duties in setting the table and caring for the dishes.

2. C and D discuss the differences between British and American customs relating to the setting of a dinner table.



Unit 98

## 1. Basic Dialogue. Caring for the lawn.

Hamisi

mkasi (MI)

scissors

ua (U)

hedge

mwiba (MI)

thorn

Nipatie mkasi wa kukatia ua wa  
mwiba.

Get me the clippers for cutting the  
thorn hedge.

Juma

nyasi (N pl.)

grass

Chukua. Ukimaliza, uje tukate nyasi  
uani.

Here you are ('take'). When you  
finish, come and we'll cut the  
grass in the yard.

Hamisi

Hapana. Wewe kata nyasi peke yako,  
mimi nina kazi nyingine.

No. You cut the grass by yourself.  
I have other work.

Juma

Kazi gani?

What work?

Hamisi

ua (MA)

flower

Maua yanahitaji kupaliliwa.

The flowers need to be weeded.

Juma

-mea

to grow

gugu (MA)

weed

Kwani magugu yamemea?

Why? Have the weeds come up?

Hamisi

Tena! Of course!

Juma

Usisahau kumwagilia maua maji. Don't forget to water the flowers.

Hamisi

-onana to see one another

Haya. Tutaonana baadaye. O.K. See you later.

Notes

## A. The reciprocal suffix.

The 'reciprocal' suffix -an- corresponds roughly to English '...one another'.

2.

## A. Concord: subject prefixes with some new nouns.

muhindi	Muhindi umemea upesi sana.	The maize has sprouted very soon.
mpunga	Mpunga umemea upesi sana.	The rice has sprouted very soon.
magugu	Magugu yamemea upesi sana.	The weeds have sprouted very soon.
ua (flower)	Ua limemea upesi sana.	The flower has sprouted very soon.
maua	Maua yamemea upesi sana.	The flowers have sprouted very soon.
nyasi	Nyasi zimemea upesi sana.	The grass has sprouted very soon.

## B. Reciprocal stems.

kuona	Wanaonana kila siku.	They see each other every day.
kupiga	Wanapigana kila siku.	They fight each other every day.
kusaidia	Wanasaidiana kila siku.	They help each other every day.
kuañkia	Wanaañkiana kila siku.	They greet each other every day.

kungoja Wanangojeana kila siku. They wait for each other every day.

C. A sentence which contains three examples of reciprocal stems.

kufuata,

kupoteza,

kuona

Hamisi na rafikiye (or:  
rafiki yake) walifuatana  
sokoni asubuhi, wakapotezana  
huko, wakaonana tena  
alasiri.

Hamisi and his friend went together  
to the market in the morning;  
they lost each other over there,  
and then saw each other again in  
the afternoon.

3.

A. Plural imperative: negative vs. affirmative.

kumwagilia Msisahau kumwagilia maua  
maji.

Don't forget to water the flowers.

Hapana. Ninyi mwagilieni  
maua peke yenu.

No. Water the flowers by  
yourselves.

kukata Msisahau kukata nyasi.

Don't forget to cut the grass.

Hapana. Ninyi kateni  
nyasi peke yenu.

No. Cut the grass by  
yourselves.

kuchemsha Msisahau kuchemsha maji ya  
kusafishia vyombo.

Don't forget to boil water for  
washing the dishes.

Hapana. Ninyi chemsheni  
maji peke yenu.

No. Boil the water by  
yourselves.

kutandika Msisahau kutandika kitanda  
cha mgeni.

Don't forget to make the guest's  
bed.

Hapana. Ninyi tandikeni  
kitanda peke yenu.

No. Make the bed by yourselves.

B. -ta- tense vs. -ki- tense.

kukata Utakata ua?

Will you cut the hedge?

Ukikata ua, nitakata  
nyasi.

If you cut the hedge, I'll cut  
the grass.

kumwagilia Utamwagilia maua maji?

Will you water the flowers?

Ukimwagilia maua, nitakata  
nyasi.

If you water the flowers, I  
will cut the grass.

kupalilia shamba kusafisha vyombo

kufua nguo

Unit 99

## 1. Basic Dialogue. Trials of a baby-sitter.

Maria

-chungu	to care for
Watoto wadogo wahitaji kuchungwa (or: kutunzwa) sana.	Young children need to be cared for very well.
-acha	to leave
Wakiachiliwa peke yao wataumia.	If they are left alone they will get hurt.
-ruhusu	to allow
-kimbia	to run
barabára	road, highway
Si vizuri kuwaruhusu wakimbie barabarani.	It's not good to let them run around in the street.
-epa	to avoid, escape
hatari (N)	danger
Hawajui kuesa hatari -- kama magari.	They don't know how to escape from dangers, like cars.
-linda	to protect
Wanataka kulindwa kila mara.	They require protection every minute.

Notes

A. The verb -ruhusu with infinitive or subjunctive.

The verb -ruhusu 'to permit' may be followed by infinitive or by subjunctive verb forms.

2.

A. Vocabulary practice in a sentence with an example of the use of the -ki- tense.

kuumia	Watoto wakiachiliwa peke yao wataumia.	If children are left alone they'll get hurt.
--------	---	---

kukimbia	Watoto wakiachiliwa peke yao watakimbia huko na huko.	If children are left alone they'll run around.
----------	---	---

kucheza      kupigana

B. -acha plus infinitive.

kusema	Wakati gani aliacha kusoma?	At what time did he stop reading?
--------	-----------------------------	-----------------------------------

kulima	Wakati gani aliacha kulima?	At what time did he stop cultivating?
--------	-----------------------------	--

kucheza      kulia

C.

kusoma	Acheni kusoma!	Stop reading!
kushangilia	Acheni kushangilia!	Stop rejoicing!
kupigana	Acheni kupigana!	Stop fighting!
kelele	Acheni kupiga kelele!	Stop making noise!
kuchemsha	Acheni kuchemsha maji!	Stop boiling water!

D. -kimbia na \_\_\_\_\_.

pesa	Watoto walikimbia na pesa zangu.	The children ran away with my money.
------	-------------------------------------	---

kalamu	Watoto walikimbia na kalamu yangu.	The children ran away with my pen.
--------	---------------------------------------	------------------------------------

kitabu      jembe      kijiko

## 3.

A. -ruhusu plus a subjunctive form; infinitive vs. subjunctive of a single verb.

kucheza	Watoto wataka kucheza barabarani. Hatuwaruhusu wacheze humo.	The children want to play in the road. We don't allow them to play in it.
---------	---	---

kukimbia	Watoto wataka kukimbia barabarani. Hatuwaruhusu wakimbie humo.	The children want to run in the road. We don't allow them to run in it.
----------	---	---

kukaa      kwenda

B. -acha and -endelea plus infinitive; mpaka.

kusema	Acha kusema! Siachi. Nitaendelea kusema mpaka usiku.	Stop talking! I won't stop. I will keep on talking until dark.
--------	--	--

kusoma	Acha kusoma! Siachi. Nitaendelea kusoma mpaka usiku.	Stop reading! I won't stop. I will keep on reading until dark.
--------	--	--

kufanya kazi      kuogelea      kukata nyasi

Unit 100

## 1. Basic Dialogue. Trials of a baby-sitter. (continued)

Mirambo

kifaranga (VI - pers.)

chick (dim.): small child  
(colloq.)

-onja

to taste, try

Vifaranga hupenda kuonja kila kitu.

Small children like to taste every-  
thing.Magese

-jali

to give honor to

Hata udongo na uchafu, hawajali.

They don't even stop at soil and  
dirt.Mirambo

jua (MA)

sun

-choma

to burn, apply fire to

Tena, watoto wa kizungu wakikaa

Also, European children, if they

juani kwa muda mrefu, huchomwa

stay in the sun for a long period,

na jua vibaya.

get badly burned (by the sun).

Magese

-tii

to obey

Watoto yawalazimu kuwatii wazazi

It's necessary for children to obey

wao.

their parents.

Mirambo

-lea

to rear



-kua

to grow

'Mtoto unileavyo ndivyo akuavyo.'

'As the twig is bent, the tree's inclined.'

2.

A. tanguJan. Hamisi amekua sana tangu  
Januari.Hamisi has grown a lot since  
January.Feb. Hamisi amekua sana tangu  
Februari.Hamisi has grown a lot since  
FebruaryMachi Aprili Mei Juni  
Oktoba Novemba Desemba

Julai Agosti Septemba

B. -kusudia plus infinitive.soko Hatukusudii kukaa sokoni  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay in the  
market long.pwani Hatukusudii kukaa pwani  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay at the  
coast long.nyumba Hatukusudii kukaa nyumbani  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay in the  
house long.kwao Hatukusudii kukaa kwao kwa  
muda mrefu.We don't intend to stay at their  
place long.Morogoro Hatukusudii kukaa Morogoro  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay in  
Morogoro long.kusini Hatukusudii kukaa kusini  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay in the  
south long.mashariki Hatukusudii kukaa mashariki  
kwa muda mrefu.We don't intend to stay in the  
east long.C. -tii

wazazi Watii wazazi wako!

Obey your parents!

waalimu Watii waalimu wako!

Obey your teachers!

mwalimu	Mtii mwalimu wako!	Obey your teacher!
baba	Mtii baba yako!	Obey your father!
mama	Mtii mama yako!	Obey your mother!

3.

A. Concord: the word mahali and the PA locative.

kalamu	Nimepoteza kalamu yangu! Mahali ulipoiacha kalamu, ndipo ilipo.	I have lost my pen! The place where you left the pen, is where it is.
pesa	Nimepoteza pesa zangu! Mahali ulipoziacha pesa, ndipo zilipo.	I have lost my money! The place where you left the money, is where it is.
kofia	Nimepoteza kofia yangu! Mahali ulipoiacha kofia, ndipo ilipo.	I have lost my hat! The place where you left the hat, is where it is.
kitabu	Nimepoteza kitabu changu! Mahali ulipokiacha kitabu, ndipo kilipo.	I have lost my book! The place where you left the book, is where it is.
chupa	Nimepoteza chupa yangu! Mahali ulipoiacha chupa ndipo ilipo.	I have lost my bottle! The place where you left the bottle, is where it is.
viberiti	Nimepoteza viberiti vyangu! Mahali ulipoviacha viberiti, ndipo vilipo.	I have lost my matches! The place where you left your matches, is where they are.

Conversation Starters

1. A (a mother) discusses with B (a baby sitter) B's responsibilities in caring for a three year old child during the day and putting the child to bed at night.

2. A (a homeowner) discusses with B (a gardener) B's responsibilities in caring for the lawn.

## READING SELECTION V

Motokaa Za Abiria

Motokaa za abiria sina manufaa sana kwa wasafiri. Ingawa abiria wapanda gari la moshi, motokaa ina sifa kabisa.

Ni ajabu kuwa safari ya motokaa si ya raha kama ile ya gari la moshi, lakini wasafiri wengi hupenda kupanda motokaa. Ukipanda motokaa, utafika upesi saidi kuliko kama ukipanda gari la moshi. Sababu yake ni kwamba motokaa yakimbia upesi saidi ya gari la moshi.

Motokaa ni nyingi sana, nazo zinasafiri kila upande nchini. Katika miji mikubwa kuna namna mbili za motokaa hisi. Zile zinazosafiri nje ya mji, na nyingine zile zinasozungukazunguka humo humo mjini. Safari nyingi huanza asubuhi na aduhuri, na chache hufanywa alasiri na jioni. Magari haya hupita katika sehemu mbali mbali, milimani na mabondeni. Juu ya mito kuna madaraja. Madaraja mengine ni membamba na mengine ni mapana. Yale membamba huruhusu gari moja moja kupita, polepole. Katika sehemu zilizo sawa, yaani zisizokuwa sa milima, magari hukimbia sana. Ni vibaya kukimbiza sana gari la abiria kwa sababu ni hatari. Wenye magari hupata faida kubwa, lakini wakati mwingine hupata hasara pia. Magari ya bidhaa, kama yale yachukusyo madebe ya mafuta, au magogo, hayachukui abiria. Hii ni amri ya serikali.

Ni wasi kwamba ukisafiri kwa motokaa, safari ndefu huwa fupi.

manufaa (pl. MA)	useful things, tools	hasara (N)	loss, damage
sifa (N)	praise, reputation	debe (MA)	a four-gallon tin
raha (N)	rest, comfort	amri (N)	a command; law authority, rule
-zunguka	to go around	wasi	open, evident
bonde (MA)	valley, low-lying country		
~embamba	narrow - thin		
~pana	broad, (flat)		

## Questions and Answers over Reading Selection

QuestionsSample Answers

- |  |   |
|--|---|
| 1. Motokaa za abiria zina manufaa kwa wasafiri?                | Ndiyo, zina manufaa sana kwao.                                  |
| 2. Je, safari ya motokaa ni ya raha kama ile ya gari la moshi? | La, si ya raha.   |
| 3. Kwa nini wasafiri hupenda kupanda motokaa?                  | Kwa sababu motokaa hukimbia upesi zaidi.                        |
| 4. Ni kweli kwamba ukipanda motokaa utafika upesi?             | Ndiyo.  |
| 5. Motokaa zinasafiri upande mmoja tu hchini?                  | La, ni nyingi sana, zinasafiri kila upande.                     |
| 6. Katika miji mikubwa, kuna namna zipi za motokaa za abiria?  | Zile zinazosafiri hje ya mji na zile zinazozungukazunguka humo. |
| 7. Safari huanza lini?   | Nyingi huanza asubuhi na aduhuri, na chache alasiri na jioni.   |
| 8. Magari haya hupita sehemu za namna gani?                    | Milimani na mabondeni.  |
| 9. Juu ya mito kuna nini?                                      | Kuna madaraja.  |
| 10. Madaraja yote ni membamba?                                 | Hapana, mengine ni mapana.                                      |
| 11. Magari hupitaje juu ya madaraja membamba?                  | Hupita moja moja, polepole.                                     |
| 12. Katika sehemu gani magari hukimbia sana?                   | Katika sehemu zilizo sawa, zisizokuwa na milima.                |
| 13. Ni vibaya kukimbisa sana gari la abiria?                   | Oh ndiyo, kwa sababu ni hatari.                                 |
| 14. Wenye magari hupata faida tu?                              | Sio faida tu, pia hasara.                                       |

15. Kwa nini magari ya bidhaa  
hayachukui abiria?

Ni amri ya serikali.

Review Sentences, Units 1 - 100

- |  |   |
|--|---|
| 1. Alinipa vitabu viwili.                          | He gave me two books.                                       |
| 2. Kimoja ni cheusi na kingine ni chekundu.        | One is black and the other is red.                          |
| 3. Mahali penyewe ni pazuri sana.                  | The place itself is very beautiful.                         |
| 4. Watoto walifika alipokuwa akila.                | The children arrived when he was eating.                    |
| 5. Mama alifika mtoto alipoanza kulia.             | The mother arrived when the child began to cry.             |
| 6. Bado hajamaliza kazi yake.                      | He hasn't finished his work yet.                            |
| 7. Alivinunua kwa shilingi hamsini na tano.        | He bought them for 55 shillings.                            |
| 8. Nijaliwapo kufika Nairobi nitamtembelea Hamedu. | If God grants that I reach Nairobi, I'll visit Hamedu.      |
| 9. Akinipunguzia bei nitakinunua kile kikapu.      | If he reduces the price for me, I'll buy that basket there. |
| 10. Suruali yako inayo mifuko mingapi?             | How many pockets do your trousers have?                     |
| 11. Mbuzi wako huko kwenye nyasi nyingi.           | The goats are where there is lots of grass.                 |
| 12. Bila shaka barabara za kwao ni nzuri sana.     | Certainly their roads are very nice.                        |
| 13. Unayo mizigo mingapi kwa jumla?                | How many pieces of luggage have you altogether?             |
| 14. Ataongea juu ya elimu ya Waafrika.             | He will speak on the education of Africans.                 |
| 15. Mimea hubadilishwa kila mwaka.                 | The crops are rotated every year.                           |

- |  |   |
|--|---|
| 16. Shamba langu limegawanywa katika sehemu tano.    | My farm is divided into five parts.                             |
| 17. Mtandikie mgeni kitanda.                         | Make the bed for the guest.                                     |
| 18. Wakulima na watoto wao walipewa msaada wa fedha. | The farmers and their children were given financial assistance. |
| 19. Yeye na dada yake wanafanana.                    | He and his sister resemble one another.                         |
| 20. Nguo avaaazo huzimunua kutoka Ulaya.             | The clothes he wears are purchased in Europe.                   |
| 21. Mwambie akuonyeshe godoro liliko.                | Ask him to show you where the mattress is.                      |
| 22. Unafikiri nguo zimelowe kwa?                     | Do you think the clothes are wet?                               |
| 23. Nani apigaye pasi nguo zake?                     | Who irons his clothes?  |
| 24. Watoto wachungao ng'ombe hawa, wako wapi?        | Where are the children who tend the cattle?                     |
| 25. Tutaondokaje hapa?                               | How will we leave here?   |
| 26. Mtapanda gari la moshi.                          | You will take the train.  |
| 27. Tutafanyaje ili tupate msaada na pesa?           | What shall we do in order to get financial assistance?          |
| 28. Baba alipofika, mama alikuwa hajaanza kupika.    | When Father arrived, Mother had not yet begun cooking.          |
| 29. Maziwa yamechemka hata yakamwagika.              | The milk boiled over.   |
| 30. Suruali haijapigwa pasi.                         | The pair of trousers hasn't been ironed yet.                    |
| 31. Mto umo ndani ya sanduku.                        | The pillow is in the chest.                                     |
| 32. Kwanini balozi hajafika?                         | Why hasn't the diplomat arrived?                                |

33. Haya, twendelee basi. O.K., let's go on.
34. Vifungo vyote vya koti lake vimepotea. All the buttons of his coat are lost.
35. Sina pesa za kuvunja noti ya shilingi ishirini. I don't have change for a 20 shilling note.
36. Duka liko kushoto kwa jumba la sinema. The shop is to the left of the theater.
37. Juzi tulikuwa tumeishiwa chakula chote. The day before yesterday, we were completely out of food.
38. Msipigane kwa sababu ya thumni. Don't fight over a 50 cent piece.
39. Hawakusudii kuja kesho kututembelea. They don't plan to come to see us tomorrow.
40. Yafaa kuwasua watoto wasichezecheze barabarani. It's necessary to prevent children from playing around in the street.



Unit 101

1. Basic Dialogue. Riding a bicycle on the streets.

Hamisi

Unajua kuendesha baiskeli?

Do you know [how] to ride a bicycle?

Abasi

Ndiyo, lakini nilianza majuzi hivi.

Yes, but I began only recently.

Hamisi

-sikiliza

to listen

sheria (N)

law

Sikiliza bwana, ni hatari sana  
kuendesha baiskeli kama hujui  
sheria za barabara.

Listen, Mister, it is very dangerous  
to ride a bicycle if you don't  
the traffic regulations.

Kila wakati endesha upande wa  
kushoto wa barabara.

Always ride on the left side of the  
road.

kengele (N)

bell

Piga kengele kama kuna mtu mbele  
yako.

Ring the bell if there is someone  
ahead of you.

-geuka

to turn

ishara (N)

signal

Ukitaka kugeuka, onyesha ishara.  
Waangalie sana wapitao kwa mguu.

If you want to turn, give a signal.  
Watch the pedestrians carefully.

Notes

A. 'Next' and 'last' with units of time.

The Swahili equivalents for 'next week', 'next month', etc. are in the form:

<u>noun</u>	<u>rel. a-tense of kuja</u>
mwezi	( ) ja ( ) o
wiki	
mwaka	

2.

A. Relative forms of the a-tense.

mguu	Waangalie sana wapitao kwa mguu.	Watch out for those crossing on foot.
baiskeli	Waangalie sana waendeshao baiskeli.	Watch for those riding bicycles.
motokaa	Waangalie sana waendeshao motokaa.	Watch for those driving automobiles.

B. Relative forms of a-tense, in time expressions.

↓	Tutaanza kujifunza mwezi ujao.	We'll begin studying next month.
mwaka	Tutaanza kujifunza mwaka ujao.	We'll begin studying next year.
wiki	Tutaanza kujifunza wiki ijayo.	We'll begin studying next week.
kupanda	Tutaanza kupanda mbegu wiki ijayo.	We'll begin sowing seeds next week.
kuvuna	Tutaanza kuvuna wiki ijayo.	We'll begin harvesting next week.
mwezi	Tutaanza kuvuna mwezi ujao.	We'll begin harvesting next week.

C. Nouns used as objects of -geuza.

maneno	Tugeuze maneno haya.	Let's change these words.
mpango	Tugeuze mpango huu.	Let's change this program.
mipango	Tugeuze mipango hii.	Let's change these programs.
majibu	Tugeuze majibu haya.	Let's change these answers.
rangi	Tugeuze rangi hii.	Let's change this color.

D. Nouns used as objects of -badili.

sheria	Tubadili sheria hizi.	Let's change these laws.
shati	Tubadili shati hili.	Let's exchange this shirt.
nguo	Tubadili nguo hii.	Let's exchange this piece of cloth.

E. The derived stem -badilishana.

koti	Tubadilishane makoti.	Let's exchange coats.
nguo	Tubadilishane nguo.	Let's exchange clothes.
kofia	kalamu	kitabu

## 3.

A. Relative forms of the a-tense.

vyombo	Vyombo vinahitaji kusafishwa. Nani asafishaye vyombo?	The dishes need washing. Who washes the dishes?
vitanda	Vitanda vinahitaji kutandikwa. Nani atandikaye vitanda?	The beds need making. Who makes the beds?
maji	Maji yanahitaji kufutwa. Nani afutaye maji?	The water needs wiping up. Who wipes the water up?
vijiti	Vijiti vinahitaji kukatwa. Nani akataye vijiti?	The bushes need cutting. Who cuts the bushes?

Unit 102

## 1. Basic Dialogue. Conditions of employment.

Sangai

Siku hizi wafanya kazi wapi?

Where are you working these days?

Wambua

fedha (N)

money

Katika Idara ya Fedha.

In the Ministry of Finance.

Twafanya kazi kwa siku tano.

We work five days [a week].

Sangai

Mshahara ni kiasi gani?

How much is the pay?

Wambua

Shilingi mia mbili hamsini.

250 shillings [per month].

Tunafanya kazi kwa muda wa saa saba.

We work a seven-hour day.

Sangai

Mnaanza lini asubuhi?

When do you begin in the morning?

Wambua

aduhuri

noon

Saa mbili mpaka aduhuri tupumzikapo.

8:00 until noon, when we rest.

Sangai

Halafu?

Then?

Wambua

alasiri

early afternoon

Halafu, tunaanza tena alasiri mpaka

Then, we begin again in the afternoon


saa kumi.

[and work] until 4.

## A. Matching hours with portions of the day.


Point to the appropriate hour as each sentence is practiced. Practice in fixed, then random order.

moja	Alifika saa moja asubuhi.	He arrived at seven o'clock in the morning.
mbili	tatu	nne
	tano	
sita	Alifika saa sita aduhuri.	He arrived at noon.
saba	Alifika saa saba mchana.	He arrived at one o'clock in the afternoon.
nane	tisa	kumi
kumi na moja	Alifika saa kumi na moja jioni.	He arrived at five o'clock in the evening.
kumi na mbili	Alifika saa kumi na mbili jioni.	He arrived at six o'clock in the evening.




3. A. What are the following in Swahili? (Assume that the sun is up.)


A.




B.




C.




D.




E.




F.




G.




H.




I.




J.



K.



L.



Unit 103

## 1. Basic Dialogue. (continued)

Sangai

Kazi yenyewe ni ngumu?

Is the work itself hard?

Wambua

afisi (N)

office

Hapana, ukiwa umeelimika, unafanya  
kazi afisini. Lakini wengine  
wanafanya kazi ngumu.

No, if you are educated, you work in  
an office. But some do hard work.

bidhaa (N)

merchandise

kadhalika

etc.

Wanabeba bidhaa kama sabuni, mafuta  
ya taa, na kadhalika.

They carry merchandise like soap,  
kerosene, and so forth.

-paka

to apply

(-pakia)

(to pile up)

Wanazipakia katika motokaa.

They load them into a lorry.

Sangai

jasho (MA)

sweat

Kweli ni kazi ya jasho!

[That] is really sweaty work.

Wambua

mapumziko

place/time of resting

Lakini sote twapewa nguo bure, na  
chakula saa ya mapumziko.

But we all are given free clothing,  
and food during the rest hour.



Sangai

bahasa (N)	envelope
karatasi (N)	paper
-omba	to request

Nitakwenda kununua bahasa na  
 karatasi ya barua ya kuomba  
 kazi kwenu. I'm going to buy an envelope and  
 letter paper for applying for work  
 at your place!

Notes

A. The stem ote 'all'.

As we have seen, the stem ote takes a full set of class concords. It also takes prefixes for first person and second person plural:

sote	we all
nyote	you all

2.

A. Subjunctive with object prefixes.

bidhaa	Ziweke bidhaa karibu na mlango.	Put the goods near the door.
bahasa	Ziweke bahasa karibu na mlango.	Put the envelopes near the door.
jembe	Liweke jembe karibu na mlango.	Put the hoe near the door.
majembe	Yaweke majembe karibu na mlango.	Put the hoes near the door.
meza	Iweke meza karibu na mlango.	Put the table near the door.

B. Relatives of me-tense and a-tense.

kuelimika	Wote waliocelimika wafanya kazi afisini.	All those who are educated work in the office.
-----------	---	---

kujua	Wote wajua kuandika na kusoma wafanya kazi afisini.	All those who know how to read and write work in the office.
kusema	Wote wasemao Kiingereza wafanya kazi afisini.	All those who speak English work in the office.
kujifunza	Wote waliojifunza Ulaya wafanya kazi afisini.	All those who studied in Europe work in the office.
kuhitimu	Wote waliohitimu wafanya kazi afisini.	All those who qualified work in the office.

C. Sote 'we all'.

kuchelewa	Tutachelewa sote.	We'll all be late.
kufurahi	Tutafurahi sote.	We'll all be happy.

kusaidia kwenda

D. Nyote 'you all'.

kuenda	Nendeni nyote.	All of you go.
kuja	Njoooni nyote.	All of you come.

kungoja kuanza kuandika

## 3.

## A. Relative with 1 plu. s.p.

kuwa	Sote tulikuwa kanisani. Sote tuliokwako tulipata homa kesho yake.	We all were in the church. All of us who were there got a fever the following day.
kuenda	Sote tulikwenda kanisani. Sote tuliokwenda huko tulipata homa kesho yake.	We all went to church. All of us who went there got a fever the following day.
kula	Sote tulikula chakula kanisani.	We all ate food in the church.

Sote tuliokula chakula  
huko tulipata homa  
kesho yake.

All of us who ate food there  
got a fever the following day.

kushinda Sote tulishinda mjini.  
Sote tulioshinda huko  
tulipata homa kesho yake.

We all spent the day in town.  
All of us who spent the day  
there got a fever the following  
day.

B. Relative with 2 plu. s.p.

kuwa Nyote mlikuwa shuleni.  
Nyote mliokuwako mlipata  
homa.

You all were in the school.  
All of you who were there got  
a fever.

kuenda Nyote mlikwenda sokoni.  
Nyote mliokwenda huko  
mlipata homa.

You all went to market.  
All of you who went there got  
a fever.

kula Nyote mlikula mjini.  
Nyote mliokula huko  
mlipata homa.

You all ate in town.  
All of you who ate there got  
a fever.

kushinda Nyote mlishinda Morogoro.  
Nyote mliosshinda huko  
mlipata homa.

You all spent the day in Morogoro.  
All of you who spent the day  
there got a fever.

Conversation Starters

1. A is looking for a good job. His friend B advises him.

Unit 104

## 1. Basic Dialogue. Rearranging the furniture.

Abasi

chumba (VI)	room
Chumba hiki kimejaa vyombo vingi visivyohitajiwa upesi.	This room is full of furniture which which will not be needed soon.
pambo (MA)	furniture, ornament
(better: <u>fanicha</u> , or <u>vifaa vya nyumbani</u> )	

Mutisya

Ni mapambo ya nyumba.	They are pieces of furniture for the house.
-----------------------	---

Abasi

Tafadhali viondoe ukipata wakati.	Please remove them when you have time.
-----------------------------------	--

Mutisya

Nitaviweka wapi?	Where shall I put them?
------------------	-------------------------

Abasi

rafu (N)	shelf
dari (N)	upper floor
Chukua rafu na kabati ndani ya chumba cha Hamisi, darini.	Take the shelf and the cupboard into Hamisi's room, upstairs.
kinanda (VI)	stringed instrument, gramophone
Kile kinanda, weka upande wa kitanda.	That musical instrument, put [it] by the bed.
kufuli (N)	padlock
ufunguo (U-N)	key
-fungu	to lock

-fungua

to unlock

Kisha, chukua kufuli na funguo hizi [When you] finish, take this padlock  
 ufunge ili watoto wasiweze kufungua. and key and lock [the room] so that  
 the children aren't able to unlock  
 [it].

Notes

## A. Negative relative present verbs.

visivyohitajiwa [things] which are not needed

The negative relative forms corresponding to the present tense have -si- in the slot between subject prefix and relative affix.

## B. The 'reversive' suffix.

kufunga to lock  
 kufungua to unlock

The 'reversive' suffix -u- is found in the word kufungua. Compare also kuvaa 'to don', kuvua 'to doff'.

## 2.

## A. Object before the verb.

kitanda Kile kinanda, weka upande That (stringed) instrument, put it  
 wa kitanda. beside the bed.

meza Kile kinanda, weka upande That (stringed) instrument, put it  
 wa meza. beside the table.

mlango kiti jiko

B. ~pi 'which' followed by relative.

vyombo Vyombo vipi visivyohitajiwa Which dishes are not wanted now?  
 sasa?

kikapu Kikapu kipi kisichohitajiwa Which basket is not wanted now?  
 sasa?

birika	Birika lipi lisilohitajiwa sasa?	Which kettle is not wanted now?				
magodoro	Magodoro yapi yasiyohitajiwa sasa?	Which mattresses are not wanted now?				
wino	Wino upi usiohitajiwa sasa?	Which ink is not wanted now?				
mkasi	Mkasi upi usiohitajiwa sasa?	Which pair of scissors is not wanted now?				
mito	Mito ipi isiyohitajiwa sasa?	Which pillows are not wanted now?				
sabuni	Sabuni ipi isiyohitajiwa sasa?	Which soap is not wanted now?				
shuka (pl.)	Shuka zipi zisizohitajiwa sasa?	Which sheets are not wanted now?				
vijiko	kitanda	godoro	mapanga	ubao	mimea	pasi
nguo (pl.)						

C. Negative relative, present tense.

kupiga	Wasiopiga kelele watapewa pesa.	Those who do not make noise will be given money.
kukimbia	Wasiokimbia watapewa pesa.	Those who do not run will be given money.
kupewa	Wasiopewa livu watapewa pesa.	Those who are not given leave will given money.
kusumbua	Wasiotusumbua watapewa pesa.	Those who do not bother us will be given money.
kuchelewa	Wasiochelewa watapewa pesa.	Those who are not late will be given money.
kucheza	Wasiocheza watapewa pesa.	Those who do not play will be given money.

kulima	Wasiolina njugu watapewa fedha na serikali.	Those who do not grow peanuts will be given money by the government.
--------	--	--

3.

A. The reversive stem -vua.

kofia	Vaa kofia hii. Usivue mpaka aduhuri.	Put on this hat. Don't take it off till noon.
suruali	Vaa suruali hii. Usivue mpaka aduhuri.	Put on these trousers. Don't take them off till noon.
nguo	Vaa nguo hizi. Usizivue mpaka aduhuri.	Put on these clothes. Don't take them off till noon.
shati	Vaa mashati haya. Usiyavue mpaka aduhuri.	Put on these shirts. Don't take them off till noon.

## B.

kofia	Vua kofia ile! Ni yangu. Kwa nini uliivaa?	Take off that hat! It's mine. Why did you put it on?
suruali	Vua suruali ile! Ni yangu. Kwa nini uliivaa?	Take off those trousers! They're mine. Why did you put them on?
nguo	Vua nguo ile. Ni yangu. Kwa nini uliivaa?	Take off that cloth! It's mine. Why did you put it on?
shati	Vua shati lile. Ni langu. Kwa nini ulilivaa?	Take off that shirt! It's mine. Why did you put it on?

Unit 105

## 1. Basic Dialogue. Planning a trip by car.

Butler

Nataka kwenda Bagamoyo kwa motokaa. I want to go to Bagamoyo by car.

Je, njia ni nzuri? Is the road good?

Hamisi

Njia ni nzuri, lakini si sana. The road is good, but not very good.

Butler

Kwa nini? Why?

Hamisi

daraja (MA) bridge

Kwa sababu juzi ilinyesha mvua kubwa, Because the day before yesterday  
na daraja moja limevunjika. there was a big rain, and one  
bridge was washed out.

Butler

Sasa nitafikaje Bagamoyo? Now how shall I get to Bagamoyo?

Hamisi

gogo (MA) log

Utaweza kufika kwa sababu watu You will be able to get there because  
wameweka magogo, na motokaa inaweza they've put logs [there], and a car  
kupita hapo polepole. can cross there [by going] very  
slowly.

## 2.

## A. N-class forms of some adjectives.

~zuri Njia hiyo ilikuwa nzuri. That road was good.



~refu	Njia hiyo ilikuwa ndefu.	That road was long.
~kubwa	Njia hiyo ilikuwa kubwa.	That road was big.
~pya	Njia hiyo ilikuwa mpya.	That road was new.

## B. LI-class forms of some adjectives.

~zuri	Bakuli hilo lilikuwa zuri.	That bowl was good.
~bovu	Bakuli hilo lilikuwa bovu.	That bowl was unfit for use.
~kubwa	Bakuli hilo lilikuwa kubwa.	That bowl was large.
~pya	Bakuli hilo lilikuwa jipya.	That bowl was new.
~chafu	Bakuli hilo lilikuwa chafu.	That bowl was dirty.
~eusi	Bakuli hilo lilikuwa jeusi.	That bowl was black.
~zito	Bakuli hilo lilikuwa zito.	That bowl was heavy.

## C. M-class forms of some adjectives.

~zuri	Mto huo ulikuwa mzuri.	That pillow was good.
~kubwa	Mto huo ulikuwa mkubwa.	That pillow was big.
~bovu	Mto huo ulikuwa mbovu.	That pillow was in a bad shape.
~pya	Mto huo ulikuwa mpya.	That pillow was new.
~chafu	Mto huo ulikuwa mchafu.	That pillow was dirty.
safi	Mto huo ulikuwa safi.	That pillow was clean.
~eupe	Mto huo ulikuwa mweupe.	That pillow was white.

## D. MI-class forms of some adjectives.

~zuri	Mito hiyo ilikuwa mizuri.	Those pillows were good.
~bovu	Mito hiyo ilikuwa mibovu.	Those pillows were in bad shape.
~pya	Mito hiyo ilikuwa mipya.	Those pillows were new.
~chafu	Mito hiyo ilikuwa michafu.	Those pillows were dirty.
~eupe	Mito hiyo ilikuwa myeupe.	Those pillows were white.

## E. U-class forms of some adjectives.

~zuri	Ubao huo ulikuwa m̄zuri.	That board was good.
~zito	Ubao huo ulikuwa m̄zito.	That board was heavy.
~bovu	Ubao huo ulikuwa m̄bovu.	That board was rotten.
~pya	Ubao huo ulikuwa m̄pya.	That board was new.
~eusi	Ubao huo ulikuwa m̄eusi.	That board was black.

## 3.

## A. Switching tense.

↓	Watu wameweka magogo.	People have put logs in place.
kesho	Watu wataweka magogo kesho.	People will put logs in place tomorrow.
sasa	Watu wanaweka magogo sasa.	People are putting logs in place now.
jana	Watu waliweka magogo jana.	People put logs in place yesterday.
bado	Watu hawajaweka magogo bado.	People haven't put logs in place yet.
waambie	Waambie watu waweke magogo.	Tell people to put logs in place.

## B. Switching tenses.

↓	Atafika Bagamoyo kesho.	He will arrive at Bagamoyo tomorrow.
jana	Alifika Bagamoyo jana.	He arrived at Bagamoyo yesterday.
tayari	Amekwisha fika Bagamoyo tayari.	He has arrived at Bagamoyo already.
bado	Hajafika Bagamoyo bado.	He hasn't arrived at Bagamoyo yet.

**jana** Hakufika Bagamoyo jana.

He didn't arrive at Bagamoyo  
yesterday.

C. Switching tenses.



Atajaza chumba mapambo  
kesho.

He will fill the room with  
furniture tomorrow.

**sasa** Anajaza chumba mapambo sasa.

He is filling the room with  
furniture now.

**jana** Alijaza chumba mapambo jana.

He filled the room with  
furniture yesterday.

**wapi** Aliyejaza chumba mapambo  
yuko wapi?

Where is the one who filled the  
room with furniture?

**sasa** Anayejaza chumba mapambo  
yuko wapi?

Where is the one who is filling  
the room with furniture?

Unit 106

## 1. Basic Dialogue (continued)

Butler

Je, mbele hakuna hatari nyingine?

Say, is there any danger ahead?

Hamisi

ajabu (N)

a surprise

Sijui, lakini si ajabu daraja la

I don't know, but I wouldn't be

Mapinga pia limsharibika.

surprised if the Mapinga bridge

is out as well.

ButlerNaweza kupata mtu mmoja wa kufuatana  
naye?Can I get someone to go along with  
me? ('one person to travel with  
him')Hamisi

iwapo

in case, if

shida (N)

difficulty

Ndiyo. Mimi mwenyewe nitaweza  
kufuatana nawe na kukusaidia  
iwapo utapatwa na shida.Yes, I myself will be able to go  
with you and help you if you meet  
difficulty.Butler

Vema. Asante sana.

Good! Thanks a lot!

Hamisi

hali (N)

condition

Kabla ya kuondoka inafaa uangalie kama gari limo katika hali nzuri.	Before leaving it's a good thing for you to check whether the car is in good shape.
---	---

Butler

Bila shaka, hata petroli nitaangalia pia.	By all means. I'll also see to the petrol.
--	---

2.

A. Si ajabu...

kuharibu	Si ajabu gari lake limeharibika.	It's no wonder his vehicle is broken down.
kutengeneza	Si ajabu gari lake limetengenezwa.	It's no wonder his vehicle is repaired.
kuzuza	Si ajabu gari lake limeuzwa.	It's no wonder his vehicle is sold.
hali	Si ajabu gari lake limo katika hali nzuri.	It's no wonder his vehicle is in good condition.

B. ~enyewe.

mimi	Mimi mwenyewe nitakwenda nawe.	I myself will go with you.
yeye	Yeye mwenyewe atakwenda nawe.	He himself will go with you.
sisi	Sisi wenyewe tutakwenda nawe.	We ourselves will go with you.
wao	Wao wenyewe watakwenda nawe.	They themselves will go with you.

C. na with personal pronouns.

sisi	Baba mwenyewe atafuatana nasi.	Father himself will go along with us.
------	-----------------------------------	--

wewe	Baba mwenyewe atafuatana nawe.	Father himself will go along with us.
yeye	Baba mwenyewe atafuatana naye.	Father himself will go along with her.
ninyi	Baba mwenyewe atafuatana nanyi.	Father himself will go along with you (pl).
wao	Baba mwenyewe atafuatana nao.	Father himself will go along with them.
mimi	Baba mwenyewe atafuatana nam.	Father himself will go along with me.

## 3.

## A. Switching tenses.

↓	Mbele naona magari.	I see vehicles ahead.
jana	Mbele niliona magari jana.	I saw vehicles ahead yesterday.
hapana	Mbele sikuona magari jana.	I didn't see vehicles ahead yesterday.
bado	Mbele sijaona magari bado.	I haven't seen any vehicles ahead yet.

## B. Questions included in a larger sentence.

gari	Gari limo katika hali nzuri? Inafaa uangalie kama gari limo katika hali nzuri.	Is the vehicle in good condition? You'd better check whether the vehicle is in good condition.
vifungo	Vifungo vimo sandukuni? Inafaa uangalie kama vifungo vimo sandukuni.	Are the buttons in the box? You'd better check if the buttons are in the box.
hatari	Kuna hatari nyingine mbele?	Is there other danger ahead?
miiba	Kuna miiba mingi njiani?	Are there many thorns on the road?

Unit 107

## 1. Basic Dialogue. In a shoe store.

Patel

Karibu, bwana.

Come in, sir!

Je, unataka viatu vya aina gani?

What kind of shoes do you want?

Butler

Ngoja niangalie kwanza.

Wait and let me look first.

Je, mna viatu vya Bata?

Do you have Bata shoes?

Patel

Oh, ndiyo, tunavyo katika rangi

Oh yes, we have them in two colors:

mbili: nyeusi na nyekundu.

black and brown.

Unataka vipi, basi?

Which do you want?

Butler

hebu

'well, then!'

mwundo (MI)

shape, form

chini (N)

below, under

Hebu nione mwundo huo chini ya  
viatu vyekundu; pia mwundo huu  
hapa.

Well, then, let me see that style  
under the brown shoes; also this  
style here.

Patel

Nitakuonyesha, bwana!

I'll show [them] to you, sir!

## 2.

A. Chini

kucheza Watoto wanacheza chini.

The children are playing on the ground.

kuanguka	Mkasi umeanguka chini.	A pair of scissors has fallen down.
kuangusha	Hamisi aliangusha sabuni chini.	Hamisi dropped soap on the ground.
kiko	Kikapu kiko chini.	The basket is on the ground.

B. Negative relative, present tense.

shati	Nataka shati lisiloraruka upesi.	I want a shirt that doesn't get torn easily.
mashati	Nataka mashati yasiyoraruka upesi.	I want shirts that don't get torn easily.
suruali	Nataka suruali isiyoraruka upesi.	I want trousers that don't get torn easily.
nguo	Nataka nguo isiyoraruka upesi.	I want a dress that doesn't get torn easily.
chandalua	Nataka chandalua kisichoraruka upesi.	I want a mosquito net that doesn't get torn easily.
vyandalua	Nataka vyandalua visivyoraruka upesi.	I want mosquito nets that don't get torn easily.

3.

A. Switching tenses.

↓	Tunavyo katika rangi tatu.	We have them in three colors.
jana	Tulikuwa navyo katika rangi tatu.	We had them in three colors.
kesho	Tutakuwa navyo katika rangi tatu.	We will have them in three colors.
sasa	Tunavyo katika rangi tatu.	We have them in three colors.



## B. Switching tenses.

	↓ Wana viatu vya Bata.	They have Bata shoes.
kesho	Watakuwa na viatu vya Bata.	They will have Bata shoes.
jana	Walikuwa na viatu vya Bata.	They had Bata shoes.
hapana	Hawakuwa na viatu vya Bata.	They didn't have Bata shoes.

## C. Switching tenses.

	↓ Mariamu anataka viatu vyekundu.	Mariamamu wants brown shoes.
kesho	Mariamamu atataka viatu vyekundu kesho.	Mariamamu will want brown shoes tomorrow.
hapana	Mariamamu hatataka viatu vyekundu.	Mariamamu will not want brown shoes.
jana	Mariamamu hakutaka viatu vyekundu.	Mariamamu did not want brown shoes.

## D. Switching tenses.

	↓ Sanduku hili limejaa viatu.	This box is full of shoes.
jana	Sanduku hili lilikuwa limejaa viatu jana.	This box was full of shoes yesterday.
kesho	Sanduku hili litakuwa limejaa viatu kesho.	This box will be full of shoes tomorrow.
sasa	Sanduku hili limejaa viatu sasa.	This box is full of shoes now.
wapi?	Sanduku lililokuwa limejaa viatu liko wapi?	Where is the box that was full of shoes?

Conversation Starters

1. A and B discuss preparations for a cross-country trip.
2. Improvise several conversations beginning with the question 'Utafanya nini kesho?'

Unit 108

## 1. Basic Dialogue (continued)

Butler

jozi (N)

pair

soli

sole

~embamba

narrow, delicate, thin

Bei gani jozi hii yenye soli

How much [is] this pair with thin

nyembamba?

soles?

Patel

Shilingi thelathini na tisa tu.

Only 39 shillings.

Butler

Na hii jozi nyingine?

And this other pair?

Patel

kuliko

where there is, than

Hii ni shilingi arobaini na sita,

These are 46 shillings, sir, because

bwana, kwa sababu jozi hii ni

this style is more attractive than

nzuri zaidi kuliko hii.

this [other].

Butler

mno

much

Lakini, bwana, bei yake ni ghali mno. But sir, their price is very high.

Patel

hafifu

poor in quality

bora

best

Ndiyo. Unajua, kitu bora siku zote  
ni ghali zaidi kuliko kitu hafifu.

Yes, you know the best (thing) is  
always more expensive than the  
low-quality stuff.

2.

A. Kinds of soles.

nyembamba Nataka viatu vyenye soli  
nyembamba.

I want the shoes with thin soles.

ngumu Nataka viatu vyenye soli  
ngumu.

I want the shoes with hard soles.

laini Nataka viatu vyenye soli  
laini.

I want the shoes with soft soles.

nzito Nataka viatu vyenye soli  
nzito.

I want the shoes with heavy soles.

mpira Nataka viatu vyenye soli  
ya mpira.

I want the shoes with rubber soles.

ngozi Nataka viatu vyenye soli  
ya ngozi.

I want the shoes with leather soles.

B. Comparisons with kuliko.

mzigo Mzigo huu ni mzito kuliko  
huu.

This load is heavier than that.

mizigo Mizigo hii ni mizito kuliko  
hii.

These loads are heavier than those.

kikapu Kikapu hiki ni kizito .  
kuliko hiki.

This basket is heavier than this.

